# UTETEZI WA MAADILI KATIKA FASIHI - NATHARI YA SHAABAN ROBERT

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

FOR USE IN THE LIBRARY ONLY

NA: ORINA B. W. MONG'ERI

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA MASTER OF ARTS KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

University of NAIROBI Library
0496771 7

Agosti, 2000

**IKRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine chochote

Orina B. W. Mong'eri

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa chuo kikuu

Dkt. Mwenda Mbatiah

Bw. Michira Nyachae

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wanangu Verah na Solomon waliozaliwa nikiwa masomoni.

# SHUKRANI

Kukamilika kwa tasnifu hii kulichangiwa na watu kadha wa kadha. Ninawashukuru wahadhiri na wasimamizi wangu Dkt. M. Mbatiah na Bw. M. Nyachae kwa kuniongoza, kunishauri na kunitia shime wakati wote nilipokuwa ninashughulikia kazi hii. Daima nilipowaendea sikukosa kupata msaada wa aina fulani ulionifaa.

Mbali na hawa nilinufaika sana kutokana na misaada ya wahadhiri kadhaa wa Idara ya Ismu na lugha za Kiafrika, hususan kitengo cha Kiswahili wakiwepo Profesa Abdulaziz, Dkt. Mutiso, Bw. Mungania, Bw. Mugullu na Dkt. Mberia. Aidha sitasahau kumshukuru Dkt. Habwe wa kampasi ya Kikuyu kwa maneno yake ya busara yaliyonifanya kujiunga na utaratibu wa mafunzo ya shahada ya uzamili.

Sitasita pia kuwatolea shukrani wazazi wangu wapendwa kwa hamasa ya hali na mali waliyonipatia, nikiwa ninang'ang'ana na kozi hii. Hali kadhalika mke wangu Pamela na watoto walinifaa sana kwa faraja zao.

Pia ninawashukuru wanafunzi wenzangu kwa mkakati tuliobuni wa kuhimizana tangu mwanzo. Vilevile sitasahau kumshukuru rafiki yangu Maroko 'Egetare' kwa aina yoyote ya msaada alionipatia.

Na mwisho ningependa shukrani zangu zimfikie Jane Wanjiru kwa kunichapishia kazi nadhifu.

AHSANTENI NYOTE

## MUKHTASARI

Tasnifu hii ni uhakiki wa utetezi wa maadili katika kazi za kinathari za Shaaban Robert. Tunashughulikia kazi tano peke yake.

Uhakiki huu unagawanywa katika sura tano. Katika sura ya kwanza tunatoa utangulizi unaohusu wasifu wa Shaaban Robert, na tafsiri ya maadili. Pia tunalieleza tatizo linalotafitiwa, na shabaha za utafiti. Aidha katika sura hii tunatoa sababu zilizotufanya kuchangua mada hii. Hali kadhalika tunataja upeo wa utafiti na kisha tunaeleza msingi wa kinadharia tuliotumia, na pia tunazirejelea kazi zilizoandikwa kuhusu mada tunayoshughulikia, na jinsi tulivyofanya utafiti wetu.

Katika sura ya pili, tunatalii aina za maadili katika kazi za kinathari za Shaaban Robert. Mosi tunazungumzia maadili ya kisiasa kabla ya kuyajadili yale ya kiuchumi na kisiasa.

Katika sura ya tatu tunaangalia namna uhusika ulivyotumiwa kuwashilishia utetezi wa maadili. Tunazungumzia wahusika wa kitaashira wenye matendo mema na maovu.

Katika sura ya nne tunatoa mambo matatu yanayoonekana kuwa nguzo muhimu katika utetezi wa maadili. Mambo hayo ni mafunzo, ushujaa na moyo wa subira.

Na sura ya tano ina matokeo ya utafiti na utoshelevu wa nadharia tuliyotumia. Sura hii pia inatoa mapendekezo kwa utafiti zaidi.

**YALIYOMO** **UKURASA**


Ikrari ..... i

Tabaruku ..... ii

Shukrani ..... iii

Muhtasari ..... iv

**SURA YA KWANZA**

1.0.0 Utangulizi ..... 1

1.1.0 Maadili ..... 2

1.2.0 Tatizo la Utafiti ..... 3

1.3.0 Shabaha ya Utafiti ..... 4

1.4.0 Sababu za kushughulikia tatizo hili ..... 5

1.5.0 Upeo wa utafiti ..... 5

1.6.0 Msingi wa kinadharia ..... 6

1.7.0 Yaliyoandikwa kuhusu tatizo ..... 9

**SURA YA PILI**

2.0.0 Aina za maadili katika kazi za kinathari za Shaaban Robert ..... 15

2.1.0 Kundi la Kisiasa ..... 15

2.2.0 Kundi la Kiuchumi ..... 22

2.3.0 Kundi la Kijamii ..... 28

Tanbihi ..... 31

**SURA YA TATU**

3.0.0 Uhusika ulivyotumiwa kuwasilishia maadili katika kazi za kinathari za Shaaban Robert ..... 32

3.1.0 Wahusika wema katika kazi za kinathari za Shaaban Robert ..... 33

3.2.0 Wahusika waovu katika kazi za kinathari za Shaaban Robert ..... 43

Tanbihi ..... 49

**SURA YA NNE**

4.0.0 Nguzo muhimu katika utetezi wa maadili katika kazi za kinathari za Shaaban Robert ..... 50

4.1.0 Mafunzo ........ 50
4.2.0 Ushujaa ........ 57
4.3.0 Moyo mwema ........ 62
Tanbihi ........ 65

**SURA YA TANO**

5.0.0 Hitimisho ........ 66
5.1.0 Muhtasari wa matokeo ........ 66
5.2.0 Utoshelevu wa nadharia ........ 69
5.3.0 Mapendekezo ........ 70
Tanbihi ........ 71
Marejeleo ........ 72

# SURA YA KWANZA

## 1.0.0. UTANGULIZI

Katika utafiti huu tunashughulikia utetezi wa maadili katika fasihi nathari ya Shaaban Robert. Ili kulikabili swala hili vilivyo, ni muhimu katika utangulizi huu kuangalia maisha ya Shaaban Robert kwa ufupi, na pia kutoa ufafanuzi mfupi kuhusu maadili.

Shabaha ya kuangalia maisha ya Shaaban Robert ni kuwa, waandishi wengi wanaamini kuwa maisha na imani za mwandishi zinatoa mchango mkubwa katika kazi zake. Mathalani Rene Wellek na Austin Warren wanasema:

> Chanzo cha kazi ya sanaa ni muumba wake - mwandishi; na tena maelezo kuhusu utu na maisha ya mwandishi zimekuwa mbinu za tangu zamani zenye misingi bora ya kutalii kazi za kifasihi.[1] (tafsiri yetu)

Malengo yetu katika utangulizi huu si kuthibitisha kauli hii ya akina Wellek, bali kudai kuwa wasifu wa Shaaban Robert una athari fulani katika kazi zake.

Shaaban Robert ni mwandishi wa nchi ya Tanzania. Alizaliwa mnamo wake wa 1909 katika kijiji cha Vibambani, yapata maili sita kusini mwa Tanga. Alikuwa mzaliwa wa kabila la Yao na daima anajitambuliza kwa lugha na utamaduni wa Kiswahili. Jina la babake lilikuwa Ufukwe. Ufukwe alikuja kuitwa Robert kutokana na jina la Mjerumani aliyeajiri babake an hivyo basi Shaaban kuitwa Robert, jina la babu yake.

Wazazi wa Shaaban Robert waliachana punde baada ya kuzaliwa kwake. Inaonekana hata hivyo, walikuwa wakikutana na mtoto Shaaban alipoendelea kukua. Mamake naye aliitwa Mwema Binti Mwidau. Walimpenda na kumwamini sana, na zaidi ya hayo walimfunza mila na desturi zao.[2]

Shaaban alioa mara mbili. Mke wake wa kwanza alipofariki alimwachia watoto wawili. Kuna kazi nyingine zinazoonyesha kuwa Shaaban Robert alioa mara tatu na alikuwa na watoto kumi.[3]

Alienda shuleni Dar es Salaam kutoka mwaka wa 1922 hadi 1926; akawa mwanafunzi wa pili katika wanafunzi kumi na mmoja waliofanya na kupita mtihani wa School Leaving Certificate mnamo mwake wa 1926 alijiunga na mtumishi wa umma kama karani. Alipendwa sana na wafanyakazi wenzake na kuheshimiwa na wakuu, wake kwa sababu ya tabia zake za kiutu na moyo mzuri. Hata hivyo, hakupandishwa cheo kutoka ukarani wala kupewa mshahara mnono. Katika tanasifu yake ya Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini, anajuta kuwa alipostaafu hakuwa na akiba ya kutosheleza mahitaji yake.

Ingawa Shaaban Robert alikuwa mtumishi wa umma, alitumia wakati wake wa ziada katika uandishi wa fasihi. Alianza kazi hii ya uandishi mwaka wa 1932. Alijiendeleza katika amali ya uandishi hadi akawa mwandishi wa Tanzania aliyetoa mchango mkubwa katika fasihi ya Kiswahili. Aliandika juu ya mambo mbali mbali: hadithi, historia, insha, magazeti, ngano, tawasifu, ushairi, wasifu wa ziwaya. Kazi zake nyingi ni za kimafumbo na hakupenda kufichwa siri ghairi ya kukusudia kalamu yake iliteleza ikazifunua.

## 1.1.0. MAADILI

Lengo letu kubwa katika kazi za Shaaban Robert limekuwa kumulika swala la uhusiano mwema miongoni mwa watu. Kwa mujibu wa V. Ferm (1957:361), maadili ni viwango dhahiri au taratibu vya mienendo miongoni mwa watu, ambamo matendo au nia za kutenda huchukuliwa kuwa nzuri au mbaya, zenye thamani au uduni na zenye ukweli au makosa.

Kutokana na fasili hii tunatambua kuwa maadili ni sifa inayopatikana tu kwa binadamu. Maadili yanahusishwa na binadamu kwa sababu ya uwezo wake wa kuyajali maslahi ya mwenzake. Kwa kuhakikisha kuwa watu wanatoa huduma zinazofaa, jamii huwa imetoa kanuni zinazoelekeza mienendo katika jamii nzima. Kanuni hizo zina uwezo wa kuyakubali na kuyapiga marufuku matendo fulani. Matendo yanayokubalika ni yale yanayoendeleza furaha, si ya mtu binafsi au kikundi cha watu, bali watu wote kwa jumla katika jamii husika. Kwa upande mwingine, yale matendo yaliyopigwa marufuku ni yale yanauyofikiriwa kukatiza furaha au maslahi ya watu wote.

## 1.2.0. TATIZO LA UTAFITI

Tatizo katika utafiti wetu linahusu uchunguzi wa dhamira ya maadili katika kazi za kinathari za Shaaban Robert.

Shaaban Robert anajitokeza kwa ushupavu katika kushughulikia dhamira ya maadili. Kazi zake za kinathari zinaonyesha kuwa anathamani utu, na utu huu una misingi yake katika maadili. Alikuwa amejitolea kufa na kupona kuhudumia jamii yake kimaadili

kupitia kazi za kinathari. Jitihada zake zinajitokeza katika Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini ambapo analalamika kuwa wachapishaji wa kazi zake hawakuwa wanamlipa haki alivyostahili kutokana na uandishi wa kazi zake. Hata alipofariki, kuna ahadi za malipo zilizokuwa hazijatimizwa.

Licha ya hayo, kazi zake za kinathari zilipochapishwa na kudhihirisha sifa ya utetezi wa maadili, alipata upinzani mkubwa kutoka kwa maadui zake. Waliendeleza vita vyao dhidi yake kupitia kwa mikutano ya hadhara na vyombo vya habari kama vile radio, magazeti na majarida. Japokuwa kulikuwa na mashambulio ya aina hiyo na matatizo mengine, Shaaban Robert hakutetereka kwa kufa moyo, bali aliendelea na uandishi wake kwa minajili ya manufaa ya jamii.

Kutokana na upinzani na vikwazo viingine, Shaaban Robert alipata nguvu mpya ya kutoa wito kwa jamii yake kudhibiti matendo yao kwa maarifa, ndipo wapate kupalilia na kudumisha maadili.

## 1.3.0. SHABAHA LA UTAFITI

Utafiti wetu una shabaha zifuatazo:

Shabaha ya kwanza ni kutambua aina za maadili yanayotetewa na Shaaban Robert katika kazi zake za kinathari. Utambuzi huo unatuwezesha kutoa hukumu inayofaa kuhusu namna maadili yalivyotetewa katika kazi hizo.

Kadhalika, utafiti huu una shabaha ya kueleza namna uhusika ulivyotumiwa kuwasilisha maadili katika kazi za kinathari za Shaaban Robert.

Pia utafiti huu una shabaha ya kufafanua nguzo muhimu zinazoonyesha utetezi wa maadili katika kazi za kinathari za Shaaban Robert.

## 1.4.0. SABABU ZA KUSHUGHULIKIA TATIZO HILI

Sababu zilizotufanya kushughulikia tatizo hili ni zifuatazo:

Tahakiki zilizofanyiwa maandishi ya fasihi-nathari ya Shaaban Robert zina upungufu wa aina moja au nyingine. Hakuna mhakiki aliyeshughulikia tatizo la utetezi wa maadili kwa kina kirefu, na kwa kutumia nadharia tunayotumia ya kisosholojia.

Shaaban Robert ni mmoja wa waandishi wa kwanza wa nathari ya Kiswahili ambaye kazi zake zinaingia katika aina ya maandishi yaitwayo "maadili" yaliyo na jukumu la kuongoa jamii. Maandishi ya aina hii yamejaa mahubiri ya mambo yenye ujumi katika jamii. Sifa nyingine ya maandishi ya "maadili", na inayojitokeza katika kazi za kinathari za Shaaban Robert ni udhihirisho wa uovu na wema, wahusika wanakuwa ama waovu kabisa au wema kamili.[4]

Aidha ni matarajio yetu kuwa mawazo yanayotokana na mada ya utafiti huu yakitumika pamoja na yale ya wahakiki wengine, yanatoa mchango wa kielimu kwa jamii yetu inayoyumbayumba baina ya ustaarabu wa kiafrika na ule wa kimagharibi.

## 1.5.0. UPEO WA UTAFITI

Utafiti huu unashughulikia maandishi ya kinathari ya Shaaban Robert. Maandishi

ya kinathari ya Shaaban Robert ni mengi na yanaweza kuingizwa katika tanzu mbali mbali. Kwa sababu zisizoepukika, tunashughulikia kazi za kinathari tano tu. Tatu kati ya kazi hizi zinaingia katika utanzu wa hadithi, na mbili zinaingia katika utanzu wa riwaya. Zile za kihadithi ni:

1. Kufikirika (1966)
2. Kusadikika (1966)
3. Adili na Nduguze (1968)

Aidha zile za utanzu wa riwaya tunazoshughulika ni:

1. Utubora mkulima (1968)
2. Siku ya watenzi wote (1968)

Lengo letu kubwa katika kazi hizi zote ni kuhakiki dhamira ya maadili.

## 1.6.0. MSINGI WA KINADHARIA

Tangu kuwe na fasihi andishi, kumetokea nadharia kadha wa kadha zinazotumiwa na wahakiki wa fasihi. Nadharia hizi zinatumiwa kama vifaa vinavyochunguza na kuhakiki maandishi ya kifasihi. Utafiti huu wetu unaongozwa na kanuni za nadharia ya kisosholojia. Nadharia hii ina sifa ya kuhusisha fasihi na jamii. Kwa vile maadili ni kipengele muhimu kinachopatikana katika jamii, nadharia ya kisosholojia inafaa zaidi kwa mada tunayoshughulikia.

Mwasisi wa nadharia ya kisosholojia anaaminika kuwa Mfaransa aitwaye Hippolyte Taine (1928-93). Taine anachukulia fasihi kuwa zao la kijamii, na anasisitiza kuwa kazi

yoyote ya kifasihi ni hati ya kijamii Wahakiki waliowahi kutumia nadharia hii wanapendekeza kuwa, ili kuelewa kazi ya kisanaa, msanii au kundi la wasanii, ni lazima tuyaelewe barabara mazingira ya kijamii ambamo msamii husika amekulia.

Mawazo ya Taine yamekuja kuwa na athari kubwa sana kwa wahakiki na waandishi wa kazi za kifasihi. Maoni yake mengi, yanaonekana kustahimili upinzani . Kwa mfano, R. Escarpit (1971:4) anasema kuwa, baada ya Taine hakuna mwanahistoria au mhakiki aliyejitokeza kupuuza uhusiano uliopo baina ya jamii na fasihi, ingawa zamani walifanya hivyo. Escarpit anaendelea kusisitiza kuwa pasipo kigezo cha kijamii, ukweli wa kifasihi hukabiliwa na mageuzo yanayoweza kulinganishwa na ramani ya dunia iliyokosa sura.

Kwa upande wake, Ngugi wa Thiongo (1978) anahusisha fasihi na maisha ya kila siku ya watu; na anatilia mkazo hoja kuwa fasihi haikui au kuchipuka katika ombwe tupu. Anaamini kuwa fasihi inapatiwa msukumo, umbo, mwelekeo na hata upeo na nguvu za kijamii. Kutokana na maoni haya ya Ngugi, tunaweza kuchukulia jamii kama kiunzi cha mifupa ambapo juu yake fasihi inajengeka. Pasipo na kiunzi hiki fasihi haiwezi kuwa na umbo mahsusi.

Mwanafasihi E. Gachukia (1980) anapendekeza, kuwa nadharia ya kisosholojia ni maarufu zaidi katika jamii zenye historia ya kutawaliwa kiuchumi, kisiasa na kitamaduni na wakoloni. Lakini hata hivyo nadharia hii inaonekana kuwa na sifa bia, kwa vile inaweza kutumika katika mazingira yoyote ya kijamii. Rainer Anorld (1973:68) anatutolea mfano wa namna inavyoweza kutumiwa kikamilifu kuhakiki kazi za kifasihi za mazingira ya

Uropa. Anasema:

> Kidesturi, mtalaa wa fasihi za kizungu unahusiana kwa karibu na mtalaa wa mazingira yao ya kijamii na mfumo wao wa falsafa na historia.
> (Tafsiri yetu)

Kuna makubaliano miongoni mwa wahakiki kuwa nadharia ya kisosholojia inatumika kitimilifu katika kuhakiki kazi yoyote ya kifasihi, ikiwa mhakiki anayaelewa mazingira ya kitamaduni ya mwandishi. Pasipo ufahamu wa mazingira ya kitamaduni ya mwandishi, tahakiki inayotokea ya kazi yake haiwi yenye haki. Wahakiki wengi wa kigeni wamewahi kutoa lawama zenye kasoro dhidi ya kazi za kifasihi za Kiafrika. Taiwo (1982:2) analalamika kuwa kasoro hizo zinatokana na udhaifu wa wageni hao, kwa sababu ya kutojua kwao misingi ya kitamaduni iliyowezesha kuandikwa kwa kazi hizo.

Wakoloni walipotawala bara la Afrika, kuna lawama nyingi za uwongo na kijinga walizotoa dhidi ya jamii ya Kiafrika kwa sababu hawakuwa wamechukua muda wao wa kutosha kujifunza mambo mengi kuhusiana na jamii yenyewe . Kwa mfano, kuna lawama kuwa kabla ya kuingia kwa wakoloni barani Afrika, Waafrika hawakuwa na utamaduni wala historia. Carrol (1980:23) anasisitiza kuwa waandishi wengi wa Kiafrika wametumia fasihi kama kigezo na kifaa muhimu cha kurekebisha walakini potofu za aina hiyo.

Kashifa zote zilizotolewa na wakoloni dhidi ya bara la Afrika hazifai hata kidogo. Hii ndiyo sababu T.S. Sengo (1973:76) kukariri mtu awaonapo, watu wa jamii nzima kuwa washenzi wa bila ya kuchunguza akaamua kuwaita hivyo, mtu huyo akichunguzwa

atakutwa kuwa mwenye dosari ya kiutu.

## 1.7.0. YALIYOANDIKWA KUHUSU TATIZO

Sio wahakiki wengi walioshughulikia dhamira ya maadili katika fasihi nathari ya Shaaban Robert. Wahakiki wengi wameshughulikia kazi za kinathari za Shaaban kwa jumla zaidi kwa kutaja mambo mengi hapa na pale. Miongoni mwa wale waliotoa mchango muhimu ni P. Mbughuni (1978), katika tasnifu yake ya shahada ya uzamifu. Katika tasnifu hii, From Oral to Written: The Politicization of Kiswahili Literature in Tanzania, mhakiki huyu ametuarifu kuwa nathari bumilizi ya Kiswahili nchini Tanzania, ilianza wakati wa serikali za kikoloni ambapo kulikuwa na haja ya maandishi ya Kiswahili kutosheleza malengo ya kielimu. Maandishi ya kwanza ya kinathari yalikuwa na sifa za fasihi simulizi, na kwa vile kazi hizo zilikuwa na malengo ya kielimu, ziliyamulikia zaidi maswala ya maadili.

Shaaban Robert alikuwa mmoja wa wale walioitikia wito wa serikali. Alishiriki kikamilifu kwa kutoa mchango mkubwa tena anuwai kuliko mwandishi yeyote wa Kitanzania wa wakati wake. Shabaha kubwa katika kazi zake nyingi ni kueneza uhusiano mwema miongoni mwa watu. Ana jitahidi kuamsha fahamu za watu juu ya wajibu wao wa kimaadili.

Mbughuni (1978:99) anaeleza kuwa kinyume cha maadili ni uovu, ambao una chanzo chake katika ukosefu wa mafunzo. Anasisitiza kuwa Hasidi na Mwivu wa Adili na nduguze, wanadhihirisha uovu kwa sababu waliyapuuza mafunzo ya kimaadili, na hivyo

basi kufanya mioyo yao kudumaa. Wanapopungukiwa na mafunzo haya wanazidi kuwa wabaya, kwa sababu uovu hupata mchanga wenye rutuba kwa wale waliokosa ufahamu wa kimaadili.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Maoni ya Mbughuni ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu yanatupa mwangaza juu ya namna Shaaban Robert alikuja kujiingiza katika uandishi. Pia yanatuarifu dhamira ilivyoshughulikiwa kwa kiasi kikubwa na maandishi ya Shaaban Robert. Shaaban Robert kushughulikia uhusiano mwema miongoni mwa watu, ina maana kuwa anahubiri maadili kwa sababu ndiyo huzalisha utu. Maadili ndiyo hutambulisha mtu kutoka kwa mnyama, na mtu yeyote aliyekosa maadili ni sawa na mnyama. Ukweli huu unatufanya kutoshangaa tunaposhuhudia Hasidi na Mwivu wakigeuzwa kuwa manyani katika Adili na Nduguze.

Mhakiki mwingine aliyeshughulikia swala la maadili katika kazi za kinathari za Shaaban ni M. Mbatiah (1999), katika tasnifu yake ya shahada ya uzamifu. Mbatiah anatutolea historia fupi ya jinsi dhamira ya maadili ilivyokuja kutokea katika kazi za kinathari za Shaaban Robert. Dhamira ya maadili inatawala sehemu kubwa ya fasihi simulizi, kwa sababu mojawapo ya malengo yake ni kuhimiza maadili miongoni mwa watu katika jamii. Mbatiah anafafanua kuwa kwa vile Shaaban anaweza kuchukuliwa kuwa mwasisi wa fasihi bunilizi ya kinathari ya Kiswahili, na mwandishi wa kwanza wa riwaya ya Kiswahili, alikuwa ameathiriwa na elementi ya kimaadili ya fasihi simulizi. Kazi za mwanzomwanzo za kibunilizi za Shaaban Robert zina uwiano mkubwa na fasihi simulizi, na tunaweza kudai kuwa fasihi simulizi ndiyo iliyotoa msingi wa riwaya ya Kiswahili.

Mhakiki huyu pia anatuarifu kuwa Shaaban Robert ni lazima alikuwa ameathiriwa

na fasihi iliyotafsiriwa hadi Kiswahili, hususan Mazungumzo ya Alfa Lela Ulela. Hadithi hizi zinadhihirisha adhabu kali kwa watovu wa maadili. Shaaban Robert anaposhughulikia maswala ya kimaadili na jinai anaonekana kupendezwa na adhabu hizo mathalani ile ya waovu kugeuzwa kuwa wanyama. Anaiona kuwa mwafaka sana katika kuwasihisha mafunzo ya kimaadili, ndiposa anaitwaa kwa matumizi katika kazi zake bunilizi za kinathari.

Tahakiki ya Mbatiah kwa maandishi ya kinathari ya Shaaban Robert imetoa mchango mahsusi katika utafiti wetu, kwa vile inatufahamisha asili ya maadili katika kazi za kinathari za Shaaban Robert. Inatuelekeza kudai kuwa Shaaban alikuwa amekulia katika mazingira yaliyokuwa kwasi katika fasihi simulizi, na alipopata uwezo wa kusoma na kuandika akatafsiri vipengele muhimu vya fasihi simulizi katika fasihi andishi. Aidha, tahakiki ya Mbatiah inatokeza kuwa Shaaban Robert alikuwa amejitahidi kudumisha maadili katika jamii yake kwa vyovyote vile, hata anapendekeza adhabu kali kwa wapotovu wasioonyeshe nia ya kubadilisha vitendo vyao viovu.

Kimani wa Njogu (1986) naye ametoa makala inayoshughulikia "Falsafa ya Shaaban Robert katika riwaya zake." Katika makala hii . Njogu anadai kuwa falsafa pana ya Shaaban Robert katika baadhi ya maandishi yake ya kinathari inahusu utu bora katika maisha ya binadamu. Njogu anasema kuwa kazi za kinathari za Shaaban Robert zinahimiza kuwa utu ni jambo la aushi linalohusu binadamu wote. Binadamu anaonekana kumiliki hulka fulani zinazompambanua na wanyama. Anasisitiza kuwa fasihi ya Shaaban Robert ni kama kioo chetu sisi kujiangalilia ili tuone tuishivyo na tunavyotaka kuishi.

Makala hii ya Kimani wa Njogu ni muhimu sana katika utafiti wetu kwa sababu inatufahamisha kuwa kazi za kinathari za Shaaban Robert hazikuwa zinalengwa kwa watu wa jamii ya Tanzania tu, bali ulimwengu mzima. Aidha umuhimu wa makala hii unadhihirishwa na pendekezo la mwandishi kuwa, kazi za Shaaban Robert ni kama kioo kinachowaelekeza watu kwa kuwaonyesha walipoenda kombo au watakapoenda kombo kwa kushiriki katika matendo fulani.

Kwa upande wake, E. Bertoncini (1989), anamwona Shaaban Robert kama mwandishi shujaa wa kazi za Kiswahili zinazoshughulikia na kuhimiza maadili. Jitihada za kushughulikia maadili zinampatia nafasi muhimu sana katika maisha ya utamaduni wa Afrika Mashariki katika karne ya ishirini. Bertoncini anatufahamisha kuwa waandishi wa "maadili" kama vile Shaaban Robert walifadhiliwa na utawala wa kikoloni, kwa sababu wao walikuwa chombo dhabiti cha kunidhamisha jamii, kwa kuihimiza kuthamini viambajengo vya maadili kama vile utiifu, huruma na mapenzi. Uandishi huu wa "maadili" haukujikita katika kazi za kiswahili tu, bali ni maudhui yaliyotamalaki miongoni mwa waandishi wengi wa barani Afrika wa kipindi hicho. Wasomi wa wakati huo walifanywa na serikali za kikoloni kuamini kuwa, lilikuwa jukumu lao muhimu kuhubiri ujumbe wa kimaadili.

Tunazidi kufahamishwa na Bertoncini kuwa, maadam maandishi yaliyotawala katika kipindi cha ukoloni yalichukua mwelekeo wa kimaadili, hata waandishi wa kidini walifinyanga, kutafsiri na kufanya ujumbe wao wa kidini kubeba maumbo ya hadithi za kimaadili ambapo wahusika waliumbwa kuchukua ama sifa za wema au uovu.

Maoni ya Bertoncini yana umuhimu katika utafiti wetu kwa kudokeza kuwa

maandishi ya kimaadili yalihimizwa na utawala wa kikoloni, kama njia mojawapo ya kuwapumbaza Waafrika. Wakoloni walijua na tayari walikuwa wameshuhudia upinzani mkali kutoka kwa Waafrika kwa sababu ya utawala wao, wa ukandamizaji. Mahubiri ya kimaadili yalikuwa kama mojawapo ya mikakati ya kunyamazisha wadhulumiwa.

Tasnifu ya Shahada ya uzamili ya R. Wafula (1989) nayo inazungumzia kazi za kinathari za Shaaban Robert. Wafula anasema kuwa Shaaban Robert ni mtu ambaye hakupenda kuona maovu katika jamii. Matarajio yake yalikuwa kuona jamii yenye usawa. Ni kutokana na hali ya kutaka usawa, tunamwona Shaaban Robert akipinga kwa ukali mfumo wa kijamii unaokandamiza wanawake, na anahimiza kuwa wanawake wanastahili kuvipinga vitendo viovu vya wanaume.

Sifa hii ya Shaaban Robert ya kutetea maadili na usawa katika jamii inamfanya Wafula kumlinganisha na Peter Abrams wa Mine Boy kwa vile wote wawili wana matarajio ya kuzaliwa kwa jamii isiyogawanyika katika misingi ya ukabila na rangi. Wafula pia anasema kuwa jitihada za Shaaban Robert katika kushughulikia maadili zinajitokeza anapotumia mbinu ya kiistiara ili kuhimiza maadili fulani, na vilevile anatumia mbinu hiyo kubeza tabia fulani potofu.

Maoni haya ya Wafula na wahakiki wengine tuliowaangalia yana uhusiano na utafiti wetu, kwa sababu yametajataja baadhi ya mambo tunavyoshughulikia katika kazi hii. Tofauti iliyoko baina ya maoni yao na kazi yetu ni kuwa, sisi tunashughulikia maudhui ya maadili kwa kina kirefu zaidi. Hata hivyo wahakiki hawa wametoa uchochezi muhimu katika utafiti wetu unaotufanya kupiga mbizi kufikia mahali walikuwa hawajafikia.

## 1.8.0. NJIA ZA UTAFITI

Utafiti huu ni wa maktabani. Tumesoma kazi zote za kinathari za Shaaban tunazoshughulikia katika utafiti huu, huku tukiangalia dhamira ya maadili. Pia tumerejelea makala mbali mbali yakiwemo majarida, tasnifu na vitabu kadha wa kadha vinavyoeleza kuhusu mada tunayoishughulikia. Kadhalika, hatukusita kutafuta ushauri kutoka kwa wataalamu wenye ufahamu katika maandishi ya Shaaban Robert.

**TANBIHI**

1. Wellek, R. na Warren, A. (1949) Theory of Literature uk.75

2. Gibbe, G.A. (1980) Shaaban Robert: Mshairi uk.66

3. Robert, S. (1968) Ashiki Kitabu Hiki uk. vii

4. Bertoncini, E.Z. (1989) Outline of Swahili LIterature: Prose Fiction and Drama uk. 35

## SURA YA PILI

## 2.0.0. AINA ZA MAADILI KATIKA KAZI ZA KINATHARI ZA SHAABAN ROBERT

Katika sura hii, tunaainisha maadili yanayoshughulikiwa katika fasili-nathari ya Shaaban Robert. Katika kushughulikia kipengele hiki kikamilifu, tumebuni makundi makubwa matatu. Kundi la kisiasa, kiuchumi and kijamii.

### 2.1.0. KUNDI LA KISIASA

Kuna wanafasihi wanaotoa dai kuwa katika miaka ya hamsini, Shaaban Robert alitoa kazi za kifasihi zilizoshughulikia maswala nyeti kama vile uhuru.[1] Wakati wa kipindi hicho wananchi wa Kiafrika walikuwa wamepata mwamko mpya wa kisiasa. Wale walioelimika, kama vile Shaaban Robert walijitwika jukumu la kupigania haki za kisiasa. Walipinga siasa za dhuluma na kudai mabadiliko katika uongozi wa kisiasa.

Shaaban Robert ni mmoja wa wale waliotumia kipawa cha uandishi wa kazi za kinathari kupigania haki za kisiasa katika jamii yake ya Tanzania. Jambo hili analiendesha kwa uangalifu bila kushambulia serikali ya kikoloni kwa njia ya moja kwa moja kwa sababu kama angefanya hivyo, kazi hizo hazingeweza kuchapishwa. Vifaa vya uchapishaji vilimilikiwa na wakoloni na walikuwa na kamati maalumu iliyopitia miswada kabla ya kuchapishwa. Miswada iliyoonyesha pingamiza kwa serikali ya kikoloni ilitupiliwa mbali. Shaaban Robert aliamua kutumia mkakati wa mafumbo katika kazi zake nyingi zinazopinga utawala kikoloni.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Kupitia kwa kazi zake za kinathari, Shaaban Robert anahimiza mabadiliko ya kisiasa. Serikali ya kikoloni inashauriwa juu ya haja ya kugeuza maongozi yake ya kisiasa yenye, dhuluma na kusambaza siasa zenye maadili, kama zile zinazodhihirishwa na baadhi ya wahusika katika kazi za kinathari za Shaaban Robert. Katika kazi ya Adili na Nduguze, Shaaban Robert anatuchorea uongozi wa kisiasa uliofaa kuigwa na viongozi wa kikoloni, na wale wa nchi huru za Kiafrika ambao hawajadhihirisha mabadiliko kamili ya kisiasa.

Shaaban Robert ametuchorea nchi ya Ughaibu inayoongozwa na Rai. Rai ni kiongozi mkamilifu mwenye sifa za upendo, usamehevu, wema, ufanyaji kazi, ukarimu. Kutokana na utawala wake mwema, binadamu, wanyama na viumbe wengine wanaridhishwa. Utawala wa aina hii unaowaridhisha binadamu na wanyama unahitaji uwezo mkubwa. Uwezo huu ndio unaomfanya Rai kuonekana tofauti sana na wafalme wengine.

Mfalme Rai wa Ughaibu ni mwenye bidii kubwa na anaweza kushiriki katika mambo mengi ya kuinua maisha ya raia wake na nchi kwa jumla. Anajitokeza kutenda kazi ndogo na kubwa kwa mikono yake mwenyewe. Badala ya kutumia mabavu na vitisho kama njia ya kufanya raia wake kutenda mambo, yeye anatumia mbinu ya ushawishi. Mbinu hii inakuwa na matokeo ya ajabu katika nchi ya Ughaibu. Imechochea raia kutenda mambo kwa hiari yao wenyewe na hivyo basi kufanya nchi kukosa watu wavivu.

Shaaban Robert pia anatuarifu kuwa baraza la Rai lilikuwa imara sana katika utoaji hukumu. Halikupendelea mkubwa wala kudhulumu aliyekuwa mnyonge. Hii inaonyesha kuwa Rai alitoa uhuru kwa mahakama kutekeleza wajibu wake bila mwingilio wowote.

Hali hii inawafanya watu wote kuwa sawa mbele ya sheria bila kuwa na upendeleo wa aina yoyote. Maongozi haya ya kisiasa yalifanya Rai kuwa tofauti sana na kiongozi yeyote aliyewahi kutawala:

> Sifa yake ilifurahiwa na viumbe wote. Malaika mbinguni waliitungia mashairi, ndege hewani waliimba kwa sauti nzuri; wanadamu duniani waliisimulia kwa hadithi; mashetani waliikariri kwa tenzi. Alikuwa mtu mmoja katika watu bora waliopata kutoka tumboni mwa mwanamke (uk. 3).

Ghairi ya uongozi wa mfalme Rai wa nchi ya Ughaibu, Shaaban Robert anatuchorea wa nchi ya Kufikirika katika <u>Kufikirika</u>. Katika mwanzomwanzo wa kazi, hii, mwandishi anatuonyesha nchi iliyokuja kustawi kwa sababu ya uongozi mwema, ingawa baadaye nchi hiyo inakabiliwa na matatizo. Nchi hii inatawaliwa na mfalme shujaa aliyejaliwa kupata nchi kubwa kuliko wafalme wengine walio majirani wake. Mfalme huyu amepigana vita vingi ili kutetea nchi yake isitekwe na maadui. Nchi yenyewe ina majeshi ya askari walio shujaa, viongozi hodari, raia wema na watiifu ambao hawalingani na wa taifa lolote lingine katika ulimwengu.

Utawala katika nchi hii ni wenye demokrasi. Tukio lolote kubwa linapatokea katika nchi, mfalme anawaita raia wake na kwa pamoja wanatafuta suluhisho linalofaa. Hali hii inadhihirika mwandishi anaposema:

> Mara nyingi tangu wakati wa mababu zangu wito wa mfalme katika Kufikirika umetiiwa na raia. Mara kwa mara wafalme na raia hapa wamekutana pamoja kushauriana juu ya mambo ya nchi; na bega kwa bega wamesaidiana kuchukua uzito wa madaraka mengi ya nchi. (uk. 5).

Shaaban Robert pia anatuarifu kuwa nchi ya Kufikirika ilikuwa ikitawaliwa kwa mujibu wa sheria. Tunaambiwa kuwa, " kulikuwa an watu hodari waliotalii sheria wenye

saburi, walikuwa ni waamuzi na wagawaji wa haki. Mahakimu hao walitenda wajibu wa kazi zao kadiri ulivyowaongoza, hawakuonyesha kwa watu nguvu za vyeo vyao." (uk. 15). Mwandishi anazidi kutueleza kuwa nchi ya kufikirika ilikuwa na serikali imara, viongozi wenye ubongo mzuri, waandishi bora, wanachuoni mufti, wasafiri na wagunduzi wavumilivu.

Uongozi wa aina hii ulifanya nchi ya Kufikirika kustawi kuliko nchi nyingine zilizokuwa jirani. Maendeleo ya nchi hii yalitokana na uongozi uliowajibika. Kulikuwa na ushirikiano uliofaa kati ya viongozi na raia.

Shaaban Robert anapiga hatua nyingine zaidi kwa kuonyesha namna utawala mwema, na hata maendeleo ya nchi vinaharibika, viongozi wanapoanza kutawaliwa na tamaa zao za kibinafsi na kupuuza majukumu yao ya kitaifa. Wao mara nyingine huanza kupinga mabadiliko yanayofaa katika kuendeleza jamii na nchi mbele. Ni jambo lisilopingika kuwa jamii daima huwa katika mkondo wa mabadiliko. Kwa hivyo inabidi viongozi na serikali kuwa tayari kukaribisha mabadiliko katika mifumo yao ya uongozi ili kuleta ufanisi zaidi katika jamii zao.

Ujinga wa mfalme wa Kufikirika unadhihirika pale anapopofuliwa na tamaa ya kupata mtoto kwa vyovyote vile. Anashughulisha raia katika jitihada za kutafuta mtoto kwa muda wa miaka sita. Shughuli hii inafanya wananchi kusahau majukumu yao ya kuendeleza nchi yao mbele. Nchi inakumbwa na matatizo makubwa ya umaskini na njaa, na wananchi kupoteza imani yao kwa serikali iliyo uongozini.

Mfalme wa Kufikirika anaonekana kuwa mtu aliyekosa maarifa kwa kushikilia

misimamo ya kizamani isiyokuwa na nafasi katika ulimwengu unaobadilika. Ingawa umri wake ni mdogo kukata tamaa ya kupata mtoto, anakosa tumaini na kuanza kuhangaika. Wasiwasi wake unatoweka wakati Utubusara, kupitia kwa maarifa yake ya elimu ya kibaolojia anamhakikishia kuwa angepata mtoto.

Kwa vile Utubusara ni mtu mwenye kisomo kizuri, anafanywa kuwa mwalimu wa mtoto wa wafalme. Mwalimu anaona haja ya kumfunza mtoto wa mfalme maarifa mapya ambayo yana lengo la kumwandaa, kuwa kiongozi wa kutegemewa katika siku za usoni. Miongoni mwa mambo mapya mwalimu anayomfunza mtoto wa mfalme, ni elimu ya kigeni na michezo. Kwa sababu ya tabia ya mfalme kupinga mabadiliko, anamwonya Utubusara juu ya kumfunza mtoto wake mambo mapya na michezo. Badala yake anatoa amri kuwa vitabu vya masomo ya mtoto wake viwe juu ya historia ya watu wa Kufikirika, habari za watu wa kale, habari za waganga, sadaka na nadhiri, uwezo wa makafara na nadhiri, uwezo wa makafara na mambo mengine duni. Mwalimu haitikii wito wa kumfunza mambo haya kwa sababu ya uwezo wake wa kung'amua mambo muhimu yanayoenda na mtaala. Mfalme anapogundua kuwa mtoto wake hafunzwi mambo aliyopendekeza anampiga kalamu mwalimu.

Ingawa katika nchi ya Kufikirika na Ughaibu Shaaban Robert ametuchorea uongozi mwema, hali anayotuchorea katika nchi ya Kusadikika ni kinyume. Katika Kusadikika anatuchorea picha ya watu waliokandamizwa na kudhulumiwa kwa muda mrefu. Watu hawa wa Kusadikika hawapewi nafasi ya kushiriki katika uongozi wa nchi. Inaonekana hata wao hawafanyi jitihada za kutosha kuhimiza serikali iliyo uongozini iwashirikishe katika utawala.

Msimamo wa Shaaban Robert katika kazi hii ya kinathari ni kwamba, hakuna maendeleo yenye maana yawezayo kuwepo ikiwa kila raia hatashirikishwa. Kazi hii iliandikwa mwaka wa 1951 wakati Tanzania ilikuwa ikitawaliwa ana Mwingereza. Ni wazi kuwa serikali za kimabavu hazikubali mawazo mapya hata ingawa mawazo hayo yataileteа tija jamii. Wazo jipya katika uongozi usiojali maslahi ya wengi huchukuliwa kuwa ni uzushi na ukiukaji wa sheria. Shaaban Robert anawashauri viongozi wawe radhi kupokea mawazo mapya ili taifa lolote lipige hatua kimaendeleo.

Inasikitisha kuwa ujumbe kutoka Kusini, Magharibi, Kaskazini, Mashariki, Mbinguni na Ardhini katu haukujadiliwa na raia wa Kusadikika bali ulikataliwa papo kwa papo na viongozi. Wajumbe walihukumiwa punde tu walipotoa ujumbe wao. Viongozi wa aina hii wanachukuliwa na Shaaban Robert kuwa watovu wa maadili kwa sababu hawawashirikishi raia katika uongozi, na wako imara kutupilia mbali mchango wa aina yoyote wa raia unaokusudiwa kuleta maendeleo katika nchi. Ukweli wa wananchi kunyimwa nafasi ya kuchangia maendeleo ya kisiasa unadhihirishwa na waziri Majivuno anapodai:

> ...... tangu zamani matendo makubwa yoyote yaliamriwa, kuanzishwa na kutendwa na watu wenye nasaba bora kama wafalme na madiwani. Watu ovyo kama alivyo mshtakiwa (Karama) hawakuachiwa kujishughulisha na mambo yaliyo zaidi ya yale yanayohusiana na maisha yao wenyewe tu (uk. 4).

Shaaban Robert anateta juu ya mfumo wa sheria uliokuwapo katika nchi ya Kusadikika. Sheria za nchi hii zilikuwa na walakini kwa kuwa na upendeleo. Sheria

zenyewe hazikuwa zinamwamuru mshtakiwa kujitetea juu ya ushahidi wa mshtaki. Aghalabu mashtaka mengi yalikubaliwa bila ya swali wala kiapo. Kama mashtaka yalitolewa mbele ya baraza na watu wenye mamlaka serikalini dhidi ya wanyonge, tumaini la kuokoka halikuweko. Dhuluma za aina hii ndizo zinazomfanya Shaaban Robert kuanzisha juhudi za kubadilisha mfumo wa kisheria katika nchi ya Kusadikika.

Kupitia kwa mhusika Karama, Shaaban Robert anawahimiza wananchi kutia bidii katika kuzipindwa sheria zilizopendelea wakoloni na kuwanyima raia haki zao za kimsingi. Baadaye juhudi za kubadilisha mfumo wa kisheria zinafua dafu elimu ya uanasheria inapokubaliwa na serikali. Mapendekezo yote ya mabadiliko uongozini yanatekelezwa na kufanya nchi Kusadikika kupiga hatua kisiasa kushinda nchi jirani.

Kazi nyingine ya kinathari inayoonyesha juhudi za Shaaban Robert katika siasa ya nchi yake na bara la Afrika ni riwaya ya Siku ya Watenzi Wote. Riwaya hii ilipoandikwa, nchi za bara la Afrika zilizokuwa zinatawaliwa na serikali za kikoloni zilikuwa zimeanza kujinyakulia uhuru. Hata ingawa uhuru ulikuwa umeanza kuingia, kulishuhudiwa michafuko ya kisiasa. Kwa mfano, kulikuwa kumetokea mauaji katika nchi ya Congo.

Shaaban Robert hakupendezwa na vurumai hizo za kisiasa. Anaonekana kuwa na hisia kuwa uhuru upatikane katika nchi za Afrika Mashariki katika wakati mmoja. Ingawa nchi hizi zingekuwa mataifa huru, Shaaban Robert anahimiza kuwa yajiunge na umoja wa aina fulani. Ni kutokana na umoja wa aina hiyo zingeweza kuyatatua matatizo yaliyozikabili. Nchi za Afrika Mashariki zilikumbwa na matatizo ya kisiasa yaliyofanana. Zote zilikuwa zimeanza kubadilisha uongozi wa kisiasa wa kikoloni kwa wa Kiafrika.

Ndoto ya Shaaban Robert inatimia wakati nchi za Afrika mashariki zilipoungana kupitia kwa Jumuia ya Nchi za Afrika mashariki ilivyokuwa na makao yake makuu mjini Arusha Tanzania.

## 2.2.0. KUNDI LA KIUCHUMI

Kundi la pili la kimaadili tunaloshughulikia katika sehemu hii ni la kiuchumi. Kazi za kinathari za Shaaban Robert zinaonyesha kuwa hali ya kiuchumi nchini Tanzania haikuwa ya kuridhisha. Nchi ilikuwa imebakia nyuma kimaendeleo. Shaaban Robert anawahimiza wananchi wenzake wafanye juhudi za kujikomboa kiuchumi. Anamshauri kila mtu binafsi na viongozi kwa jumla kuwa, maendeleo yanategemea bidii za matendo yetu. Katika Adili na Nduguze anasisitiza kuwa:

> Kula uhondo kwataka matendo.
> Asiye matendo hula uvundo. (uk. 28).

Aidha Shaaban Robert anatimiza wajibu wake wa kijamii kwa kuwafahamisha wenzake kuwa, wanastahili kufanyia vipawa vyao kazi kikamilifu, ndipo wapate kuepukana na hali ya umaskini. Anawaarifu kuwa, maumbile yalikuwa si bahili bali karimu vya kutosha katika kugawa vipawa. Lakini zaidi ya nusu ya hasara za wanadamu hutokea kwa sababu wenyewe hawataki kutumia vipawa vyote walivyopewa. Katika kazi hii ya kinathari, Shaaban Robert anatuonyesha namna nchi ya Ughaibu ilivyokuja kuendelea kutokana na bidii za mfalme Rai. Bidii zake zilishawishi raia kutumia vipawa vyao.

Watu wanaelezwa umuhimu wa kuweka hesabu wanapoendelea na shughuli zao za kiuchumi. Viongozi wanajulishwa kuwa nchi zilizopata hatua kimaendeleo zilikuwa na

viongozi waliokuwa waangalifu kuhusu michango ya kuendeleza nchi zao. Shaaban Robert anatutolea mfano wa Rai ambaye hakukoma kutazama hesabu za wanyama waliokusanywa kwa kodi. Ni kutokana na makini hii alipata kugundua kuwa karibu mazizi yote katika miliki yake yalikwisha lipa kodi zao ila mazizi ya Janibu. Anapotambua kasoro hiyo, hapotezi wakati kwani anaanzisha uchunguzi.

Pia Shaaban Robert anatueleza kuwa ingawa ufanisi wa Adili ulitokana na bidii, alikuwa mwangalifu katika uwekaji hesabu. Tunaambiwa kuwa hakuacha kuhesabu kitu alichokinunua au alichokiuza. Vitu vyote vilivyoingia ndani na vilivyotoka nje, alivitia daftarini kwa uangalifu. Hali hii ndiyo inayomwezesha kutambua kuwa baada ya mwaka mmoja amepata mali iliyo sawa na iliyoachwa na baba yake.

Katika kazi ya kinathari ya Kufikirika, Shaaban Robert anatueleza kuwa ufanisi wa awali wa nchi ya Kufikirika ulitokana na bidii za wananchi katika utendaji wa kazi. Isipokuwa watoto, Wafikirika wote walikuwa na desturi ya kufanya kazi kwa muda mrefu kuliko watu wote katika mataifa mengine ya dunia. Watu wa mataifa mengine walipokuwa wamo katika usingizi, uvivu, anasa na uzembe, Wafikirika walikuwa katika mashindano ya kutenda mambo makubwa na yaliyokuwa bora kuliko wenzao.

Kazi kubwa katika nchi hii ilikuwa ni ukulima, ufugaji, uhunzi, useremala, uashi, uganga na nyinginezo. Kila mfanyakazi wa aina fulani alitakiwa awe stadi. Kwa mfano, mkulima alitakiwa awe stadi na mwelewa wa kila njia ya ukulima na nyakati mbalimbali za kazi hiyo. Kutokana na mfano huu wa kazi za Kufikirika, Shaaban Robert anawahimiza wafanyakazi mbalimbali katika nchi yake watafute maarifa zaidi katika kazi wazifanyazo.

wapatapo ustadi katika kazi zao, uzalishaji ungeongezeka na hivyo basi kugeuza hali zao za kiuchumi.

Shaaban Robert anatoa wito kwa watu wa jamii yake kuwa punde wanapoanzisha juhudi za kufanya kazi, wasivunjike moyo. Kuvunjika moyo kunaleta hasara mbaya. Anawaonya kupitia janga lililoipata nchi ya Kufikirika wakati watu walipoacha kazi zao kwa muda wa miaka sita, huku wakitafuta tiba kwa ugumba wa mfalme. Nchi ambayo zamani ilikuwa na shibe, utajiri, tafrija and neema zote iligeuka kuwa yenye njaa, umaskini, uchi, uzito na uhitaji wa kila namna.

Tunapoangalia kazi ya kinathari ya <u>Kusadikika</u>, tunaona Shaaban Robert akifafanua kuwa, hakuna maendeleo ya kiuchumi yoyote yawezayo kuwepo katika taifa ambamo umma unaozalisha mali unatawaliwa na mabarakala wachache wanaomiliki vyombo vya kuzalisha mali. Tunaarifiwa kuwa kina mama wa Kusadikika walizaa mapacha. Hii ni jazanda ya iktisadi ya Kusadikika, kwamba iliJaa malighafi. Hata hivyo malighafi hii haikufurahiwa na umma kwa sababu haukupewa nafasi.

Mathalani mjumbe wa kaskazini, Buruhani anatoa rai ya kukutanisha bidii za taifa la Kusadikika katika shabaha moja. Anataka maendeleo ya nchi yachangiwe na kila mtu kwa ushirika wa kazi, fikira na mali. Ushirika huu unakusudiwa kuendelea mpaka Kusadikika istawi kama nchi nyingine. Shauri hili linapowekwa mbele ya serikali halikukubalika. Wajumbe kutoka maeneo mengine wanapotoa yale maendeleo waliyoyaona katika safari zao, serikali inayapuuza na kuwatia kifungoni. Hali hii inafanya nchi na raia wake kudumaa kiuchumi.

Viongozi hawa wa Kusadikika wanaweza kuchukuliwa kuwa walikosa maono ya kiuchumi kwa sababu baada ya ushindi wa Karama, mafanikio makubwa yanapatikana:

> Baada ya miaka michache kupita mafunzo yote yaliyotolewa Kusadikika na wajumbe yaliamsha bidii zilizokuwa zimelala. Mavuno ya mafunzo hayo yalifanyiza Kusadikika kuwa nchi moja katika nchi zilizostawi kabisa (uk.57).

Katika riwaya ya Utubora Mkulima, Utubora amechorwa kama kielelezo cha kile Shaaban Robert akionacho kuwa chenye fahari. Anamwachisha Utubora kazi ya mshahara mkubwa huko Unguja na kumrudisha mashambani kufanya kazi ya ukulima. Msimamo wa Shaaban Robert ni kwamba, ukulima ni shina la maendeleo ingawa unadharauliwa na wasomi-teule. Amedhamiria kuitwaza hadhi ya ukulima ili yeyote aifanyaye kazi hii (au anayekusudia kuifanya) asijione duni.

Katika nchi nyingi za Kiafrika, ukulima unachangia sehemu kubwa la pato la kitaifa. Kutokana na kilimo kuna viwanda mbali mbali vinavyojengwa na kuajiri idadi kubwa ya watu. Mishahara inayopatikana huinua hali ya maisha ya watu na pia huchangia maendeleo ya kitaifa. Bila kilimo maisha hayawezi kudumu. Kilimo ndicho kinacholishwa watu wa taifa lolote. Ikiwa watu wana njaa, hawataweza kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi yao.

Maisha ya mashambani na ukulima yanatiliwa maanani na Shaaban Robert kupitia kwa Utubora. Utubora akiwa anaendelea na kazi yake ya ukarani, anaingiwa na ufahamu

kuwa, miji mikubwa inachangia maangamizo ya watu, ambao kwa haraka ya kujitafutia fahari na vyeo vyao wenyewe, huwa hawaoni kusudi la Muumba Kuwa watu walilazimu kuishi katika ulimwengu, kwa kula matunda ya ardhi. Utubora anakuja kushangazwa na namna alivyoweza kuzivumilia dhiki za mji kwa siku nyingi. Anaingiwa na hamu ya kwenda Mrima na kutengana na fahari ya mambo ya mjini bila ya sikitiko. Fahamu zinapomwingia kuwa maisha yaliyokuwa yanamkonjea yangekuwa na sifa kama za babu yake wa kwanza, Adamu, anafurahi kuliko alivyokuwa zamani.

Hatua ya Utubora kuingilia kilimo inakuwa na mvuto mkubwa kwa Radhia. Ingawa Radhia ametoka katika familia tajiri inayopuuza ukulima, yeye haoni ubaya wa mtu kuwa mkulima. Sababu hii ndiyo inayomfanya kuvunja uchumba na Makuu na kuamua kuolewa na Utubora. Shaaban Robert anaonyesha namna matajiri wanavyochukia ukulima kupitia kwa chungu unaowaingia wazazi wake Radhia. Wazazi wa Radhia wanaona ukulima kama kazi ya watu maskini na ndiyo maana wanasikitikia binti yao anapofikia uamuzi wa kuolewa na Utubora. Lakini Shaaban Robert anasisitiza kuwa kama kilimo kilikuwa kazi mbaya, basi haingeweza kufanywa na kufurahiwa na babu wetu Adamu.

Shaaban Robert anaiona kazi ya kilimo kuwa bora zaidi kuliko kazi nyingine yoyote. Katika Kufikirika mtu mjinga na mwerevu wanapohitajika kwa kafara ya kuponya mtoto wa mfalme, Utubusara anachaguliwa kuwa mjinga kwa sababu ya kazi yake kuwa ukulima. Kwa upande mwingine, mtu anayechaguliwa kuwa mwerevu ni mfanya biashara. Shaaban Robert anapinga kigezo kilichotumiwa kuchagua watu hawa. Anasema:

> Kama watu wa biashara ni werevu, wasingepata hasara katika kazi yao, na kama wakulima ni wajinga njaa ingefuta asili ya mwanadamu juu ya uso wa ardhi (uk. 45).

Ni jambo la kutia moyo kuwa baadaye, mkulima aliyedhaniwa kuwa mjinga anatokea kuwa mwerevu na mfanya biashara mjinga. Mkulima aliyechukuliwa kuwa mjinga anajitokeza kuwa mwenye mantiki inayookoa maisha yake na ya mwenzake. Utubora ndiye anayetoa suluhisho la kumponya mtoto wa mfalme. Shauri lake ni kuwa mtoto wa mfalme apelekwe hosptalini kutibiwa. Kwa hakika baada ya matibabu mtoto anapona.

Kupitia kwa kisa hiki cha Utubusara, na uamuzi wa Utubora kuacha kazi ya ukarani na kuingilia ile ya ukulima, Shaaban Robert anawashauri vijana wa nchi yake ya Tanzania na bara la Afrika kwa jumla kuwa, ukulima ni kazi adilifu na waupe stahiki yake na wasikakawane na kulowela mijini. Lakini hali hii ni lazima ifungamanishwe na muktadha wa mifumo ya kiiktisadi na kijamii isababishayo vijana kutoka mashambani na kulowela mijini. Tatizo la Shaaban Robert ni kwamba hatuonyeshi migaragazo, mikinzano na mivutano ya kiiktisadi ilundikizayo viwanda; inayoruhusu mabwanyenye kuweka hifadhi ya mashamba yasiyofanyiwa kazi; na inayotoa elimu finyu isiyo ya kujitegemea bali ya kumwezesha mtu afanye kazi ya ukarani kama Utubora, elimu inayomtayarisha mwanafunzi awe msomi-teule.

Kwa kumalizia tunaweza kusema kuwa katika sehemu hii tumeangalia namna Shaaban Robert anavyowashauri watu wa jamii yake kuwa, umaskini na matatizo mengine yanaweza kuepukwa kwa jitihada za ufanyaji kazi, na utunzaji wa mapato yao.

Kwa mfano, anaonya:

> Watu watumiao mali zao kwa ubadhirifu husemwa kuwa wametumbukia katika maangamizi ya matumizi. Mwisho watu hao huvunjwavunjwa katika maanguko ya umaskini, yaani njaa, kiu na nchi. Watu watumiao mali zao kwa uangalifu huyaepa maanguko ya umaskini--- Hazina kubwa hufanywa kwa kukusanya senti moja moja kama safari ndefu ifanywavyo kwa mwendo wa hatua moja moja.[2]

## 2.3.0. KUNDI LA KIJAMII

Katika sehemu hii tunaangalia maswala ya kijamii yanayoshughulikiwa katika kazi ya kinathari za Shaaban Robert. Shaaban Robert amejitolea sana kuona kuwa kuna mahusiano mema baina ya binadamu na binadamu, na pia baina ya binadamu na viumbe wengine. Katika mahusiano haya, binadamu ndiye anayechorwa kuwa na wajibu muhimu, kwa vile ana uwezo maalumu wa kujali maslahi si yake tu, bali hata ya viumbe wanaomzunguka.

Nia ya Shaaban Robert kupigania mahusiano mema kati ya binadamu na viumbe, inawasilishwa na mfalme Rai wa nchi ya Ughaibu. Mfalme huyu zaidi ya kuthamini utu, alithamini pia maisha na ustawi wa wanyama. Inapogunduliwa na Ikibali, mshauri wa mfalme, kuwa uhusiano kati ya Adili na manyani wawili haukuwa mzuri, anaonyesha haja ya kutaka kujua sababu na papo hapo anaanzisha juhudi za kumpatanisha Adili na wanyama wake.

Katika Kufikirika, Shaaban Robert anasisitiza kuwa jamii yake ilitilia maanani uzazi.

Uzazi unathaminiwa katika jamii hiyo kwa sababu ndivyo njia ya pekee ya kuendeleza maisha ya binadamu. Mtu yeyote aliyekosa uwezo huu alidharauliwa na jamii, na yeye mwenyewe kukosa utulivu wa akili. Dai hili linathibitika kuhusiana na wasiwasi aliyokuwa nayo mfalme ilipomchukua muda mrefu bila kupata mtoto. Mfalme analitoa tatizo lake hadharani. Raia wanamsikitikia na wanachukua hatua ya kuacha shughuli zao ili wapate suluhisho kwa tatizo la mfalme.

Riwayani Utubora Mkulima, Shaaban Robert anatahadharisha jamii juu ya athari ya fedha katika kuvuruga maadili. Kupitia kwa kinywa cha nguli wake anasema:

> _ _ _ sidhani kuwa fedha huweza kukidhi matilaba yote; ingawa mtu ni lazima kuwa na kiasi fulani cha fedha ya kumsaidia na kumpatia mahitaji yake ya kawaida bali hutia utumwani maisha ya mtu (uk. wa 59).

Ili kueleza wazo lake kuwa fedha hazipaswi kumwondolea mja ubinadamu na haki zake, ameonya kwamba ndoa isifungamanishwe na mali, bali ifuate hisia za maharusi. Anashutumu kitendo cha Sheha kumtoroka Utubora na kuolewa na mtu mwenye fedha. Ndoa hii haikudumu kwa sababu ilikuwa imejengeka katika msingi wa fedha. Kuna baadhi ya wahusika kama vile Makuu ambao maisha yao yanaongozwa na fedha. Makuu mathalani anakariri kuwa bila fedha mwanamume hawezi kuoa hata mwanamke anayempenda.

Katika kazi za kinathari za Shaaban Robert, pia tunaona akihimiza watu kumcha Mungu. Anawashauri kuwa in jambo adilifu kwa binadamu kumtambua Muumba wake.

Anaonya kuwa, binadamu asipoishi na kutenda mambo kulingana na mapenzi ya Mungu, hana budi kuangamia. Katika Adili na Nduguze, Shaaban Robert anatoa kisa chenye dhamira ya kilichoupata Mji wa Mawe kwa sababu wakaaji wake na mfalme waliabudu mizimu. Kwa mfano, mfalme wa mji huo anakufuru mtume wa Mwenyezi Mungu kwa kumwambia:

> Nini kilichokujusurisha kusema upuzi, mrefu? Kama kwa sababu ya urefu ubongo wako umeyeyuka kwa jua, kaa kitako chini ya kivuli cha mizimu yetu utaburudika (uk. 37).

Kujitolea nafsi kwa mambo ya Mwenyezi Mungu, kunapanuka zaidi katika Siku ya Watenzi Wote, ambapo Shaaban Robert anainyemelea dini impe suluhisho kwa matatizo yote ya kijamii. Nguli wake Ayubu, hatibu wa Jumuia ya Adili, anaamini kuwa matatizo ya ulimwengu yametokana na binadamu kutotoa zaka, sadaka na ushuria. Mahubiri haya ya Shaaban Robert yanatokana na ukweli kuwa alikuwa mwislamu, na ndipo akaona haja ya kuwafundisha watu wa jamii yake mambo ya Mungu.

Hali kadhalika, katika riwaya ya Siku ya Watenzi Wote, tunaona Shaaban Robert akishutumu mifumo ya kijamii katika nchi yake iliyokuwa ya ukandamizaji. Anapinga mila na ada zilizopendelea wanaume na kuwanyanyasa wanawake. Hata sheria za nchi zinaonekana kuwapa wanaume uwezo wa kuwanyanyasa wanawake. Ukandamizaji wa wanawake unadhihirika katika sura ya kwanza, ambapo kuna kisa cha mtu aliyemtoroka mkewe kurudi nyumbani na kumpura kwa makonde mpaka anazirai. Mtu huyo anapopelekwa mahakamani anahukumiwa kifungo cha siku moja na nusu au faini ya shilingi mbili; ilhali kuna kisa kiingine ambapo mwanamke alitupa rungu dirishani akalivunja, na mahakama ikampa adhabu ya kifungo cha miezi mitatu na kazi ngumu. Hakimu ambaye

alikuwa mwanaume alidai kuwa kama mtu alikuwa nyuma ya dirisha hilo angaliumizwa.

Shaaban Robert anateta kuwa mfumo wote wa kijamii na kisheria katika jamii yake ulihitaji mabadiliko. Katika mabadiliko hayo wanaume na wanawake wangekuwa sawa. Sheria pia ingeweza kuhudumia watu kwa usawa bila kuwapendelea wanaume. Mabadiliko hayo ya sheria ndiyo yangempatia mwanaume wajibu wa kumlinda na kumtetea mwanamke.

**TANBIHI**

1. Bertoncini, E. Z. (1989) OUTLINE OF SWAHILI LITERATURE uk. 39.

2. Robert, S. (1966) Kusadikika uk. 35

## SURA YA TATU

## 3.0.0. UHUSIKA ULIVYOTUMIWA KUWASILISHIA MAADILI KATIKA KAZI ZA KINATHARI ZA SHAABAN ROBERT

Uhusika katika kazi za kinathari za Shaaban Robert una sifa za kiistiara. Istiara ni mtindo katika fasihi ambao kwao vitu au watu husimamia dhana au wazo maalumu.[1] Majina ya wahusika katika kazi za kinathari za Shaaban Robert, hususan zile za mwanzomwanzo yanaashiria maana fulani na wala hayakupachikwa kiholela. Maana za majina haya zinahusiana na matendo au tabia za jumla za wahusika hawa. Kwa jumla, kazi za kinathari za Shaaban Robert zina wahusika wa aina mbili; waadilifu na maovu. Wale waadilifu wamepatiwa majina yanayoashiria wema, ilhali wale waovu wamepatiwa majina yanayoashiria uovu.

Kutokana na ithibati tuliyo nayo, mtindo wa kiistiara katika kazi za kinathari za Shaaban Robert umetumiwa kwa wingi sana katika kazi za mwanzomwanzo na kufifia katika kazi za baadaye. Mojawapo ya sababu zinazofanya mbinu ya kiistiara kujitokeza zaidi katika kazi za awali kuliko za baadaye ni kuwa, athari ya fasihi simulizi bado ilikuwa na nafasi muhimu katika nafsi ya Shaaban Robert. Istiara ni mbinu ya kifasihi inayotumiwa zaidi katika fasihi simulizi kuliko fasihi andishi. Kwa vile Shaaban Robert ni mmoja wa waanzilishi wa fasihi bunilizi ya Kiswahili, bila shaka alikuwa na hiba ya fasihi simulizi.

Matumizi ya vipengele hivi vya fasihi simulizi ni thibitisho fika kuwa, kazi hizo za kinathari zililenga watu wa jamii ya Shaaban Robert. Na katika kuwahudumia vilivyo, kama inavyodhihirika katika nadharia yetu ya kisosholojia, ilimbidi Shaaban Robert kutumia

mbinu zilizoeleweka na kufahamika na jamii yake. Ikiwa angetumia mbinu za kigeni basi kazi hizi zingepata wasomaji wachache. Kwa kushughulikia kipengele cha sura hii kikamilifu, inatubidi kushughulikia wahusika wazuri kwanza katika kazi zote kabla ya kuingilia wale waovu.

### 3.1.0. Wahusika Wema Katika Kazi Za Kinathari Za Shaaban Robert

Katika Adili na Nduguze, kuna mhusika Rai. Kwa mujibu wa Kamusi Sanifu ya Kiswahili, neno "rai" lina maana nne, ambapo tatu zinahusiana na maadili. Kwanza, rai lina maana ya kusema na mtu kwa maneno mazuri kwa madhumuni ya kumtaka akubali kutimiza linarotarajiwa. Pili, rai lina maana ya hali ya mwili kuwa na afya nzuri; na tatu, rai lina maana ya wazo au maoni ya mtu juu ya jambo fulani. Maana hizi tatu zina uwiano na matendo au sifa za mfalme Rai wa Ughaibu.

Mfalme Rai haonekani kuwa kiongozi anayetumia mabavu anapotaka raia kutekeleza wajibu wao wa kibinafsi na wa kitaifa. Anawashawishi na kuwabembeleza kupitia kwa matendo yake. Mbinu hii inaonekana kuwa na athari kubwa kwa raia kwa vile wote wanaiga kiongozi wao. Raia wote wanaacha tabia ya uvivu na kujitolea kwa kutenda yaliyo mema. Mfalme Rai pia anadhihirishwa kuwa mtu asiyekosa mapendekeza mema. Kwa mfano, anapogundua kuwa ndugu wake Adili walikuwa wanyama, anampendekezea Adili jinsi angevyoweza kuwaokoa kutoka adhabu ya unyama. Ingawa mapendekezo yake mwanzoni yanaonekana kuwa magumu kwa Adili, yanapotekelezwa ndiyo yanayookoa Hasidi na Mwivu.

Kadhalika, Rai anajitokeza kuwa mkwasi kwa maarifu na akili ya kuweza kudhibiti

hata majini. Yeye ndiye anayeongoza mkataba unaoleta maelewano baina ya pande mbili zinazozosana yaani binadamu na majini. Anajitolea kuandikia Huria binti Kisasi barua inayowawezesha Hasidi na Mwivu kuwa binadamu tena. Kila Shaaban Robert anachohimiza kupitia kwa Rai ni kuwa mtu anayestahili kuongoza watu ni yule aliye na uwezo mkubwa kutatua matitizo ya watu anaowaongoza.

Adili ni mhusika mwingine ambaye jina lake linaashiria uadilifu. Neno 'adili' lina maana ya mwenendo mwema usio na mapendeleo. Pia lina maana ya maonyesho au mafunzo yatolewayo kwa namna ya hadithi au shairi yakiwa na nia ya kufundisha. Aidha lina maana ya kutenda haki.[2] Adili hakupewa jina hili bila sababu mahsusi. Alipewa jina hili ili awe mfano bora wa mtu mwadilifu ambaye inafaa aigwe na kila mtu. Maana za 'adili' ambazo tumetoa hapo juu zinaoana na tabia na matendo ya Adili. Adili amejitolea kutenda mema kufikia kiwango cha kujiadhibu kimwili na kisaikolojia. Mwandishi ametutolea mfano wa mahali ambapo Adili anakosa kuwacharaza ndugu zake na anacharazwa vilivyo na majini. Tumeonyeshwa pia huruma aliyokuwa akiwaonea ndugu zake punde alipoanza kuwacharaza. Alijutia makosa yao.

Ingawa Adili ni mtu mwadilifu, anayefanikiwa kwa chochote akifanyacho, mara nyingine anakabiliwa na majaribu. Majaribu hayo hayawi ya kudumu kwani baadaye yanashindwa. Kushindwa kwa majaribu hayo ni taashira ya nguvu za maadili dhidi ya maovu.

Katika kazi ya kinathari ya Kusadikika, majina ya wahusika wema yanaashiria uadilifu sawa na ilivyo katika Adili na Nduguze. Mfalme wa Kusadikika ambaye ametajwa

kiheshima tu kama 'Jalali.' anajitokeza kuwa mwadilifu kutokana na hatua yake ya kumpa Karama nafasi ya kujitetea kwa muda wa siku sita, wakati wengine walitaka kesi yake iamuliwe siku hiyo hiyo. Isitoshe, mfalme huyu anadhihirisha kuwa 'Jalali' kamili, katika uamuzi wake wa mwisho kuwa karama hana hatia.

Ushindi wa Karama unakuwa mwanzo wa kuleta mabadiliko katika nchi iliyokuwa imepinga mageuzo kwa muda mrefu. Wajumbe sita waliokuwa wanaangamia gerezani wanafunguliwa na jumbe zao kutekelezwa, hali inayoleta ustawi mkubwa katika nchi. Kutoka wa vitendo hivi, inakuwa wazi kuwa mfalme huyu ni mtu anayependelea mabadiliko. Swali tunaloweza kujiuliza ni je, mbona mabadiliko haya yalikosa kutokea mwanzoni? Labda ni kuwa mfalme alizidiwa nguvu na washauri wake mpaka alipofikia uamuzi wa liwe liwalo. Au pengine alizidiwa nguvu na upinzani wa wanaharakati na kwa kuhofia mapenduzi akalegeza msimamo wake wa awali wa kupinga mabadiliko.

Nguli katika <u>Kusadikika</u> ni karama. Karama lina maana ya kipawa au uwezo wa namna ya pekee anaokuwa nao mtu kwa sababu ya kumwabudu Mungu. Karama anaelezwa na kuthibitisha kuwa na vipaji vya hekima, ushujaa na umbuji. Shaaban Robert hatuambii kama vipaji hivi alizaliwa navyo au vilitokana na kujifunza. Vitendo vya Karama vinadhihirisha kujitolea kwake kuwahudumia watu kama inavyoashiriwa na jina lake. Kujitolea kwake kunaonekana kwa namna anavyotetea wajumbe waliofungwa bila hatia. Anakuwa mkombozi wao. Fauka ya hayo, kujitolea kwa Karama kunadhihirika anapoanzisha elimu ya Uanasheria na kujitolea kwake kuwafunza watu umuhimu wa elimu hiyo. Mwishowe, tunapopata kuwa kile Karama anachokipigania kimetimia, inaonyesha kuwa uhusika wake katika kesi hiyo ngumu, na jina lake vilipata baraka kutoka kwa

Mwenyezi Mungu. ushindi wa karama pia unatokana na utetezi wenye mantiki na uwezo wa kuwavuta watu kwa umbuji wake.

Karama ni mtu mwenye adabu. Ingawa anajua kuwa ana vipaji vyake vitatu, havitumii kwa njia isiyofaa. Anavitumia kwa uangalifu pale tu vinapohitajika, na hii ndiyo sababu hata marafiki zake hawajui kama anavyo. Hali hii inamfanya kuwa tofauti na wahusika wengine wenye vipaji ambao hujigamba hadharani. Hawezi kulinganishwa na Majivuno kwa mfano, anayejisifu kuwa ana hekima kutokana na umri wake mkubwa na tajriba yake serikalini. Karama ni mnyenyekevu kiasi cha kutoweza kuvuta nadhari ya mtu.

Wajumbe wote sita wa Kusadikika wana majina ya kiistiara yenye kuashiria sifa za kimaadili. Majina yao yote ni ya Kiislamu na yana uhusiano wa namna fulani na Mwenyezi Mungu. Mjumbe wa Kaskazini alikuwa Buruhani. Buruhani lina maana ya uwezo wa Mwenyezu Mungu au kipaji kinachotolewa na Mwenyezi Mungu. Safari ya Kaskazini ilikuwa ni ndefu sana na yenye dhiki chungu nzima. Watu walipojaribu kuifikiria, walihofia maisha yao na hawakuwa tayari kujitolea. Wakati watu walipokuwa karibu kukata tumaini la kupatikana mjumbe kwa safari hiyo, ndipo Buruhani anajitokeza. Kujitolea kwa Buruhani kunakuwa kama bahati kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kwa sababu anatokea wakati nchi inapohitaji msaada.

Mjumbe wa Mashariki alikuwa Fadhili. Fadhili lina maana ya utoaji msaada wakati haja shida. Mikasa iliyomkumba mjumbe wa kwanza, Buruhani wakati na kabla ya safari yake ilikuwa imesimuliwa. Watu walimsikitikia kwa yote yaliyompata. Inapofikia wakati nchi inahitaji mjumbe mwingine kwa safari ya Mashariki ni lazima raia waliogopa kuwa

wasije wakapatwa na majanga kama yale yalivompata Buruhani. Lakini majanga hayo havakumvunja Fadhili moyo. Anajitolea kuhudumia nchi yake.

Mjumbe wa Kusini alikuwa Kabuli. Kabuli lina maana ya ukubalifu wa dua au maombi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kabuli alikuwa anayafahamu mateso wajumbe waliotangulia walikumbwa nayo safarini, na ukatili waliopata kutoka kwa serikali; kwa vile ujumbe wao ulikataliwa na wao kutiwa gerezani. Kabuli anajitolea kwa safari ya Kusini akiwa na matumaini kuwa ujumbe wake ungekubaliwa na serikali.

Safari ya Magharibi ilifanywa na Auni. Auni lina maana ya nusura au tegemeo. Auni anapojitolea kwa safari yake ya Magharibi, ujumbe wa watangulizi wenzake ulikuwa umekataliwa. Safari ya Auni inaonekana kama tegemeo lililobakia kuinusuru nchi yake.

Mjumbe wa Mbinguni alikuwa Ridhaa. Ridhaa lina maana ya hali ya kukubali au kutosheka na jambo. Ridhaa anaonekana kutosheka na namna serikali ya Mbinguni ilivyoendesha. Anakuwa na tumaini kuwa ujumbe wake ulitosha kuleta mabadiliko yaliyofaa nchini mwake.

Mjumbe wa mwisho alikuwa Amini. Amini lina maana ya kusadiki au kukubali. Amini ana imani kuwa kwa vile ujumbe wa wenzake waliotangulia ulikataliwa, wake ungekubaliwa. Pia ana imani kuwa ujumbe wake ungetekelezwa, nchi yake ingepiga hatua kimaendeleo.

Kazi ya kinathari ya Kufikirika ina majina machache ya wahusika yanayoenda sambamba na tabia za wahusika. Nguli katika kazi hii ni Utubusara. Utubusara ni mhusika mwadilifu, na mwenye busara kama jina lake linavyoashiria. Shaaban Robert anatuarifu kuwa ingawa taifa la Kufikirika linajitokeza kuwa na ustawi mkubwa, lina nuksi, kwa sababu mfalme hana mrithi. Kwa kutumia maarifa makubwa, Utubusara aliye mkuu wa watabiri, anaibuka na utabiri wa kuzaliwa kwa mtoto wa mfalme. Maarifa anayotumia katiba utabiri huu ni ya elimu ya kibaolojia inayopendekeza umri ambao mtu anafikia na kupoteza tumaini la kupata mtoto. Malkia na mfalme walikuwa chini ya umri huo, ndiposa Utubusara anatabiri kuwa wangepata mtoto.

Mtoto wa mfalme anapozaliwa, Utubusara anatumia busara kuajiriwa ualimu wa mtoto huyo. Anaitumia nafasi hii kueneza na kusakifisha maarifa mapya nchini, kwa kumfunza mtoto huyo elimu ya kigemi. Katika mtaala wa elimu ya mtoto huyu, Utubusara anaongeza michezo. Mtaala wenyewe unamfanya mtoto wa mfalme kudhihirisha uwezo mkubwa masomoni. Utubusara anapofutwa kazi, na mtoto kulazimishwa kufuata mtaala tofauti usiokuwa na michezo masomoni, mtoto anakuwa mgonjwa kwa sababu alipewa kazi nyingi na hali ubongo wake ulikuwa mchanga kuhimili mambo mengi.

Busara ya Utubusara inamwelekeza katika ukulima na kuchaguliwa awe kafara ya kumponya mtoto wa mfalme. Kupitia kwa Utubusara, Shaaban Robert anashutumu kafara ya binadamu kwa kushauri kuwa mtoto angepona ikiwa angepelekwa hospitalini kupata matibabu. Ushauri huu unaonyesha kuwa watu wa jamii ya Shaaban Robert walishikilia ukale, jambo linalomsukuma Shaaban Robert kuwafahamisha kuwa walihitajika kubadilisha hali yao ya maisha na itikadi zilizopitwa na wakati.

Ni kutokana na busara. Utubusara anajinusuru na kumnusuru mwenzake ambaye wangechinjwa naye. Hapa tunaweza kuona kuwa Utubusara alikuwa ametumia mshale wa busara kuyafuma mawazo yaliyopinga elimu ya kigeni. Shaaban Robert anatuhimiza kupitia kwa Utubusara kuwa twende kwa henezi na busara endapo twataka kubadili nafsi zetu. Heba anayoipata Utubusara baada ya kujinusuru na kumnusuru mwana wa mfalme ni ishara ya faida inayoletwa na mabadiliko.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Nguli katika riwaya ya Utubora Mkulima ni Utubora. Kupitia kwa mhusika huyu, Shaaban Robert anawasilisha kile anachokiamini kuwa uadilifu katika maisha ya binadamu. Utubora anatoka Unguja na kwenda Burma kushiriki katika vita. Anapoondoka kwenda Burma, tayari amemposa binti wa tajiri wake, Sheha. Utubora anaporejea kutoka Burma, anapata kuwa Sheha amemtoroka na kuolewa na mtu tajiri. Anafanya kazi yake ya ukarani kwa tajiri wake wa zamani kwa muda mfupi na kuhamia Mrima (mashambani), mahali ambapo anaamini kuna uadilifu. Huku mashambani anakutana na watu wema kama wile Radhia na Bimkubwa. Akiwa anaishi mashambani, anajaribu kujichukua kwa namna isiyowaudhi watu wengine.

Shaaban Robert amemchora Utubora kama mtu mwadilifu. Uadilifu wake unajitokeza anapoitikia wito wa serikali yake kwa kujiunga na jeshi ili kwenda kushiriki katika ukombozi wa watu waliokuwa wanadhulumiwa katika mazingira ya mbali. Muda wote alipokuwa Burma alizidi kukuza mapenzi yake juu ya Sheha, ingawa kwa upande wake Sheha, anakuwa msaliti kwa kumtoroka. Aidha Utubora akiwa mashambani, anasaidia kubadilisha hali ya Bimkubwa, aliye na simanzi kwa kuwapoteza watu wote wa

jamaa yake na sasa anaishi maisha ya upweke. Huzuni unamfanya Bimkubwa kukata tamaa ya maisha. Anaamua kujifungia nyumbani na kujitenga na watu. Haoni maana hata ya kustawisha kiunga chake. Lakini kupitia kwa juhudi za Utubora, hali ya Bimkubwa inabadilika kuwa nzuri. Anampenda na kumwona Utubora kama mwanawe. Shaaban Robert anampatia Utubora jina lingine la 'Mkulima' kuonyesha fahari yake katika ukulima. Ile nadharia inayohusisha ukulima na adhabu iliyotolewa na Mungu kwa binadamu kwa sababu ya uasi, haionekani kumwathiri.[4] Pia Shaaban Robert anaonekana kupinga maisha ya mjini kwa sababu anayaona kuchangia uovu katika jamii. Mapenzi ya Shaaban Robert kwa ardhi yanaonekana kutokana na jina la mahali anakomhamishia Utubora, 'Busutamu'.

Ingawa kupitia kwa Utubora Shaaban Robert anaonyesha mapenzi aliyo nayo kwa kilimo, Utubora pia anakuwa kielelezo cha aina nyingine ya maadili: uvumilivu, uaminifu na bidii. Utubora anapofanya kazi kwa tajiri wake, Ahmed, anadhihirisha uvumilivu kwa majaribu yaliyoangamiza jamii yetu ya leo kama vile rushwa. Tajiri wake pia anafurahishwa na uaminifu aliokuwa nao Utubora mpaka akafikiria kumfanya mshirika katika biashara yake. Utubora pia anajitokeza kuwa mtu mwenye bidii kazini: ndiye mtu wa kwanza kuhudhuria na wa mwisho kutoka.

Shaaban Robert amemtumia Utubora kueleza msimamo wake kuhusu uhusiano unaotarajiwa baina ya matajiri na watumishi wao. Anasisitiza kuwa ni jambo adilifu kuwa na uhusiano mwema. Anapinga hali ya matajiri kuwaona watumishi wao kama vifaa vya kufanya kazi na wala sio kama binadamu. Uhusiano unaoonekana kati ya Bihaya na Utubora ni wa kuridhisha. Wao wanaaminiana, kuheshimiana na kuwajibiana. Wote wawili wanashirikiana katika kutafuta suluhisho kwa maswala nyeti. Kwa mfano, Utubora

anapotaka kuhama Unguja anamfahamisha Bihaya, halafu kunazuka mjadala baina yao. Inadhihirika kuwa Shaaban Robert hakupendezwa na namna matajiri wazungu walivyowatendea wafanyakazi wao wa Kiafrika. Hakukuwa na wakati maoni ya Mwafrika yalisikizwa na tajiri wake mzungu.

Utubora amedhihirisha ukamilifu wa mja. Ameonyesha sifa za kiutu kama vile kuwa safi kimwili na kiroho, kuwa na heshima kwa wenziwe, kuwa na akili nzuri na pia kuonyesha kuwajibika. Ingawa mara nyingine anaonyesha kuchanganyikiwa kwa sababu ya matatizo yanayomkabili, lakini anajikaza kuishi kulingana na msimamo wake. Anaishi na kujichukua kwa namna inayomtosheleza binafsi na pia inayokubalika na watu wanaomzunguka.

Radhia ni mhusika mwingine aliye mwadilifu. Jina Radhia linatokana na 'radhi'. Radhi lina maana kutosheka na matendo ya mtu. Radhia anaonyesha wasiwasi kuhusiana na upweke wa Bimkubwa. Anamhurumia na kumwombea hali yake ibadilike haraka. Jitihada za Utubora kubadilisha hali ya Bimkubwa zinapofua dafu, Radhia anatosheka. Radhia pia anatosheka na tabia na ukamilifu wa Utubora, hali inayomfanya kumwacha Makuu na kuolewa na Utubora.

Riwaya ya Siku ya Watenzi Wote ni kazi nyingine ya kinathari inayotubidi kuangalia uhusika wake. Riwaya yenyewe inayoshughulikia maisha ya kijamii nchini Tanzania kipindi kifupi baada ya uhuru. Jamii ya kipindi hicho ilijengeka katika misingi ya kitabaka. Kuna matabaka mawili makubwa: walivyo navyo na wasivyo navyo. Tabaka la walivyo navyo ndilo linalomiliki mali na kuongoza serikalini. Tabaka la wachochole

linakumbwa na matatizo mengi ambayo mengine yanaonekana kuchangiwa na serikali.

Shaaban Robert kupitia kwa wahusika wake wakuu, anajaribu kutafuta suluhisho la kudumu kwa matatizo yanayoikumba jamii yake na ulimwengu kwa jumla. Wahusika wakuu katika riwaya hii ni kama mwanasheria Yusuff; Ayubu Chuma Akili; Binti Akili, shangaziye Ayubu; Sarah, mtoto wa binamuye Binti Akili na Izak. Wahusika hawa wanadhihirishwa kuwa waadilifu kwa vile, kwa njia, moja au nyingine wanashiriki katika utatuzi wa matatizo katika jamii yao. Ayubu ni mwanzilishi wa Jumuia ya Adili ambayo kutokana na Shaaban Robert ingekuwa suluhisho kwa matatizo yote yaliyoikumba jamii yake. Jumuia hii inakusudiwa kuunganisha dini zote na kutawala tofauti za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Lengo kubwa katika muungano huu ni kuboresha maisha duniani na kuandaaa watu kwa maisha yajayo.[5] Ayubu anazunguka jijini Dar-es-Salaam na viungani mwake akitimizia maskini mahitaji ya kimwili na kihoro kama maandalizi ya maisha jayo.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Yusuff ni mwanasheria aliyeenda ng'ambo kusoma kwa miaka kumi. Anaporudi nchini mwake anashuhudia mabadiliko makubwa. Nchi iliyokuwa ikitawaliwa na wakoloni sasa imekuwa huru, lakini uhuru huo hautoi matumaini yoyote kwa wachochole. Anapotembezwa na kuhudhuria mikutano kadha ya Jumulia ya Adili huku akitoa michango yake kusaidia maskini, anaamini kuwa Jumuia hii ndiyo ingekuwa suluhisho la pekee kwa matatizo ya baada ya uhuru. Hatua ya Yusuff kupongeza Jumuia ya Adili ina maana kuwa shirika hili lilikuwa limeanza kuwa maarufu kwa kuwavutia hata wasomi.

Mhusika mwingine mwadilifu ni Saraha. Sarah ni kijana wa karibu miaka kumi na mitano, lakini aliye na mali nyingi. Anawasikitikia maskini na anawasaidia kwa michango

yake ya ukarimu. Hata anapendekeza kutoa vyote alivyo navyo kwa Jumuia ili kuwanufaisha maskini. Lakini Ayubu anamjulisha kuwa kanuni ya Jumuia inamruhusu mtu kutoa ushuria tu.

Binti Akili naye ni mwanamke mchangamfu na tena mkarimu. Ni mmoja wa wale wanaotoa michango ya hali na mali kwa Jumuia ya Adili. Inaonekana anapendwa na watu kwa sababu mara nyingi watu hawakosi nyumbani kwake. Izak ni mhusika mwingine mwadilifu. Ingawa mwanzoni Shabaan Robert anatuchorea picha inayotoa hisia kuwa ni mtu mbaya, lakini baadaye vitendo vyake vinaonyesha kuwa ni mtu mwema. Kwa mfano, ana toa mchango mkubwa katika kukomboa sufuria za Kimbaumbau zilizokuwa zimechukuliwa na mla riba.

### 3.2.0. Wahusika Waovu Katika Kazi Za Kinathari Za Shaaban Robert.

Katika kazi zake za kinathari, Shabaan Robert ametumia wahusika wenye tabia na matendo maovu. Tunapolinganisha idadi ya wahusika wema na wale waovu, ile ya wahusika wema inazidi. Hili ni dhihirisho kuwa Shabaan Robert anapatia maadili uzito maalum. Wahusika wakuu waovu katika kazi ya Adili na Nduguze Hasidi na Mwivu.

Matendo ya wahusika hawa ni maovu kama inavyoashiriwa na majina yao. Hasidi ni mtu mwenye uchoyo kwa ufanisi wa wengine. Mwivu naye ni mtu mwenye uchoyo unaotokana na mapenzi ya watu wawili. Hasidi na Mwivu wanaweza kubadilishana majina kwa vile matendo na fikira zao ni sawa. Wao binafsi wanataka kila kitu kizuri bila ya kufikiria juu ya ndugu yao. Kwa mfano, nia ya kumtumbukiza ndugu yao majini ni kumtaka mpenzi wake na mali yote aliyojipatia kutoka Mji wa Mawe. Maangamizi ya uhasidi na

wivu yanajitokeza kupitia kwa vita vinavyozuka baina yao, kwa vile kila mmoja wao anamtaka mpenzi wake Adili, ambaye awali walipendekeza wamwoe kwa ushiriki. Ushirika waliopendekeza unageuka na kuwa ubinafsi.

Tabia za Hasidi na Mwivu haziwi tofauti na za wanyama. Hawana hata chembe cha utu. Wanaoneka kuwa wazembe, waliokosa uangalifu katika matumizi ya fedha. Kwa sababu ya kupenda anasa, wanaharibu mali nyingi waliyoachiwa na baba yao, na mwishowe wanakuwa fukara. Wakati wowote walipolemewa kwa umaskini walimwendea ndugu yao kwa usaidizi, naye aliwasaidia vilivyo. Lakini tena inashangaza wanapotaka kumwua. Watu hawa hawana hisia zozote za kijamii. Kile kilichoharamishwa na jamii, wao wanakiona kuwa halali. Upotofu wao ndio unaowaongoza kupendekeza kumwona Mwelekevu kwa ushirika; jambo ambalo halijawahi kushuhudiwa katika jamii ya Kiafrika.

Shaaban Robert amewatumia Hasidi na Mwivu kupiga vita tabia fulani zisizokuwa na nafasi katika jamii yake, ambazo huenda zilikuwa kawaida katika jamii za kontinenti nyingine. Kwa mfano, ilisemekana kuwa katika bara la Asia, mwanamke mmoja angeweza kuolewa na wanaume wengi. Shaaban Robert anashutumu tabia ya aina na kusisitiza kuwa, ni ya kinyama isiyostahili kuonekana katika jamii yoyote ya kibinadamu.

Ufuasi wa dini ya Kiislamu unamfanya Shaaban Robert kukashifu watu wanaoabudu mizimu. Mojawapo ya mihimili muhimu ya dini ya Kiislamu ni utambuzi wa Mungu mmoja. Ibada ya mizimu inachukuliwa kuwa tendo la kikafiri linalohitaji kukabiliwa kwa jihadi. Janga hili ndilo linampata mfalme Tukufu na wakaaji wa Mji wa Mawe. Katika Uislamu, mfalme anachukuliwa kuwa mwakilishi wa Mwenyezi Mungu

duniani. lakini mfalme Tukufu anakufuru agizo hili na kumfanya Mwenyezi Mungu kuangamiza kila kitu katika mji huo isipokuwa Mwelekevu aliyekuwa mwadilifu.

Uhusika wa majini katika kazi ya kinathari ya Adili ya Ndunguze ni wa kiistiara na unashirikishwa na uovu. Mjeledi na Huria wanadhihirisha kiburi walicho nacho majini. Mjeledi ukiwa na maana ya kiboko kinachotokana na ngozi, hauvunjiki kwa urahisi. Uhusika wa Mjeledi katika kazi hii unaashiria ugumu na ukaidi wa majini katika kubadirisha uamuzi wao. Ukaidi wa majini unaonekana Hasidi na Mwivu wanapoadhibiwa. Hawaonewi huruma hata kidogo mpaka Rai anapongilia kati. Huria ni binti wa kijini. Jina lake linaashiria uhuru alio nao. Uhuru wake unaonyeshwa anapowaadhibu Hasidi na Mwivu bila ya kushauriana na wazazi wake juu ya adhabu inayofaa. Kupitia kwa Huria, Shaaban Robert anapinga uhuru usio na mipaka kwa sababu huwa chombo cha kuendeleza maovu katika jamii.

Katika Kusadikika, kuna mhusika Majivuno aliye waziri mkuu. Majivuno lina maana ya kiburi au maringo. Majivuno amechorwa kuwa mtu anayejisifu kwa madaraka alivyo nayo. Anayatumia madaraka yake kuwaangamiza wale wanaofanya juhudi za kuleta mabadiliko katika nchi ya Kusadikika. Haileweki sababu zilizomfanya Shaaban Robert kumwumba mhusika huyu kwa namna ambavyo kwa kiwango fulani, anaonekana kuwa mwema na kwa kiingine mwovu. Tunaarifiwa kuwa Majivuno ana haiba na uhodari. Neno haiba lina maana ya kuvutia. Kuvutia kunaweza kuwa ama kuwa tabia nzuri au mbaya. Kadhalika, Majivuno kuwa 'hodari' inaweza kuwa na maana ya uhodari kwa utendaji mema au maovu.

Majivuno pia anadhihirishwa kuwa na kipaji cha umbuji. Kipawa hiki ndicho kinachomsaidia kutekeleza malengo yake ya tadi na inda kwa kuwaangamiza wanaharakati wa mabadiliko nchini Kusadikika. Anakitumia kipaji hiki kutanza na kuthibitishia baraza kuwa wanaharakati hao ni waasi wasiohitaji huruma ya baraza. Maarifa na juhudi zake zinalenga kuwaangamiza wanaharakati kwa sababu ya kuhofia kuwa walikuwa tisho kwa cheo chake. Alikuwa tayari kumnasa hata Karama kama mfalme hangeingilia kati.

Kuna wahusika wadogo wanaoshikilia madaraka serikalini ambao ni waovu. Taadabuni ni katibu wa baraza. Jina lake lina maana ya kumfunza mtu adabu kwa njia ya kumshusha kiheshima. Komeni ni jina linalotokana na 'koma', linalomaanisha kukomesha kitu. Akiwa amiri jeshi wa Kusadikika, anakomesha juhudi zote za wapinzani wa serikali. Taadabuni na Komeni wanaashiria nguvu zinazopinga raia kufurahia haki yao ya kujieleza. Fujo lina maana ya ghasia au mchafuko. Mhusika huyu akiwa mweka-hazina wa Kusadikika, anaashiriwa kutumia vibaya rasilimali za nchi yake. Boramimi ambaye ni mkuu wa sheria anaonekana kuwa na ubinafsi mwingi. Hata tafsiri anayeitoa ya uanasheria ni ya kibinafsi zaidi.

Katika kazi ya <u>Kufikirika</u>, kuna mfalme wa nchi ya Kufikirika ambaye anadhihirika kuwa na ubinafsi mwingi. Ubinafsi huu ndio unaomfanya kujilundikia mali ya kitaifa ambayo ingetumiwa kwa faida ya raia wote. Anajisifu kuwa:

> Nina mali katika hazina inayoweza kununua kitu chochote kinachopatikana kwa thamani kubwa katika soko za dunia bila ya kuonyesha upungufu. Hazina hizo zimejaa tele fedha, dhahahabu, almasi, yakuti, zumaridi, feruzi, johari n.k. (uk.2).

Ubinafsi wake pia unaonekana pale anaposhughulisha watu kwa tatizo la kibinafsi. Watu wanalazimika kuacha shughuli zao za kiuchumi kwa muda wa miaka sita kutafuta tiba ya kumpatia mtoto. Ubinafsi huu unatumbukiza nchi katika janga la umaskini. Mfalme huyu pia anaonekana kuwa mtu aliyekosa maarifu na utulivu maishani. Mbona anakosa tumaini la kupata mtoto na hali umri wake ulikuwa mdogo?

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Waziri mkuu wa Kufikirika pia anajitokeza kuwa mwovu. Uovu wake unaonekana pale anapotumia kifua kuhalalisha kafara ya binadamu kinyume na ilivyo katika katiba. Anatumia mabavu kubadilisha katiba ili kutimizia mfalme haja yake ya kibinafsi. Pia ameeleza kuwa mwenye hasira, wivu, hila na choyo kikubwa cha mamlaka. Mara nyingi alilazimisha wanachama wa baraza waliompinga kustaafu au kuacha kazi.

Kazi ya kinathari ya Utubora Mkulima inamdhihirisha Makuu kuwa mhusika mwovu. Kama inavyoashiriwa katika jina lake, yeye ni mtu anayejitakia makuu. Ni kutokana na sifa hii tunamwona akishangazwa na hatua ya Utubora kuacha kazi nzuri huko Unguja kwa ajili ya kazi ya ukulima anayoiona kuwa ya mashaka. Licha ya hayo, Makuu anaonekana kuthamini fedha kuliko kitu kiingine chochote. Anaamini kuwa mtu akiwa na pesa hawezi kuwa na shida yoyote. Imani yake kwa fedha ndiyo inayomfanya kushuku upweke wa Bimkubwa kwa sababu alikuwa na fedha nyingi. Anamsingizia kuwa na kiranga.

Ingawa Makuu anaonyeshwa kuwa mwenye fedha, Shaaban Robert hatuonyeshi namna alivyokuja kuwa na fedha hiyo. Anawaonya wale watu wanaoamini katika fedha kuwa wabadilishe hisia zao kwa sababu fedha haiwezi kutosheleza haja zote za binadamu.

Sawa na Makuu. Sheha ni mhusika mwingine anayethamini fedha. Sababu hiyo ndiyo inayomfanya kumwacha Utubora na kuolewa na mtu tajiri. Katika kuonyesha udhaifu wa fedha katika maisha ya jamii, Shaaban Roert anaonyesha namna ndoa kati Sheha na mume wake tajiri haikuwa ya kudumu.

Kazi ya Siku ya Watenzi Wote inayo wahusika wadogo walio waovu. Mfano mzuri ni wa mwajiri wa Bi Nunu. Mtu huyu ni mdhalimu. Anataka kumnyima Bi Nunu pesa zake na hata kumfuta kazi kwa sababu zisizokuweko. Anasingizia kuwa kazi ya bibi huyu ilikuwa mbaya na hali alikuwa ameifanya kitaalamu. Ukweli ni kuwa, anamdhulumu kwa sababu ya kuwa mwanamke. Mfumo mzima wa kijamii unaonekana kuwadhulumu wanawake. Kazini, walikuwa wakifanyizwa kazi kwa muda mrefu lakini malipo kidogo. Hali hii inamwudhi Shaaban Robert na kuwahimiza wanawake kupiga moyo konde na kuanza kutetea haki zao.

Tabia ya mwajiri wa Bi Nunu inalingana na ya mla riba. Mla riba naye anataka kumnyang'anya Kimbaumbau sufuria zake kwa sababu ya kuwa mwanamke. Mtu huyu ni mfisadi kwa sababu kina Sarah wanapompatia pesa zake hazitaki. Inawabidi kutumia nguvu ili kukomboa sufuria hizo.

Kwa jumla katika sura hii tumejadili namna uhusika ulivyotumiwa kuwasilishia maadili katika kazi za kinathari za Shaaban Robert. Kuna vipengele viipingine vinavyochangia uwasilishaji wa maadili katika kazi hizi ambavyo hatukuweza kuvigusia kwa sababu kama tungevigusia, basi ingalitubidi tuliingilie swala zima la fani ambalo halikuwa lengo letu katika sura hii.

Tunaweza kuhitimisha sura hii kwa kusisitiza kuwa kazi za kinathari za Shaaban Robert zinaonyesha matumizi ya wahusika wema na waovu. Matumizi ya wahusika wa namna hii yana lengo la kuonyesha mgogoro uliopo baina ya maadili na maovu. Kwa sababu lengo la Shaaban katika kazi hizi ni kuhimiza maadili, vitendo vyenye maadili vimejitokeza kuwa na nguvu kwa kushinda vile viovu.

**TANBIHI**

1. Masoko, D. na Mdee, J. (1984) MULIKA uk. 39

2. Kamusi ya Kiswahili Sanifu

3. Kama nambari ya 2.

4. Biblia Takatifu na Koran

5. Wafula, R. (1989) The use of Allegory in Shaaban Robert's Prose Works uk. 78

## SURA YA NNE

## 4.0.0. NGUZO MUHIMU KATIKA UTETEZI WA MAADILI KATIKA KAZI ZA KINATHARI ZA SHAABAN ROBERT

Katika sura hii tunayaangazia mambo muhimu yanayompatia Shaaban Robert uchochezi wa kutetea maadili katika jamii. Mambo hayo ndiyo yanayokuwa nguzo muhimu ambamo vita vya Shaaban Robert dhidi ya maovu vimejengeka. Vita dhidi ya maovu katika kazi za kinathari za Shaaban Robert vimejengeka katika nguzo tatu muhimu: mafunzo, ushujaa na moyo mwema.

### 4.1.0. MAFUNZO

Elimu ni kitu muhimu katika jamii. Mtu apatapo elimu mawazo yake yanapanuka, na anaanza kuvipatia vitu mtazamo mpya. Kwa njia nyingine, tunaweza kuona elimu kama ufunguo wa akili. Mtu anaweza kupata mafunzo kupitia utaratibu uliozoeleka wa kujiunga na shule au kupitia kwa njia iliyo nje ya utaratibu. Shaaban Robert alikuwa amepata elimu kupitia kwa njia mbili tulizozitaja. Katika utangulizi wa kazi hii tulitaja kuwa ingawa wazazi wa Shaaban Robert walikuea wametengana, walikutana naye mara kwa mara kumfunza mila na desturi zao.

Hali kadhalika, katika wasifu wa Shaaban Robert, tuligusia kuwa alikuwa mmoja wa wanafunzi waliopita mtihani wa School Leaving Certificate. Elimu hii, ile aliyoipata kutoka kwa wazazi wake na tajriba yake ya maisha vyote vilichangia kumfunza maadili. Haiwezekani kuwa mtu anaweza kufahamu taaluma fulani bila ya kupata mafunzo. Kutokana na kazi za kinathari za Shaaban Robert tunaweza kudondoa mifano ya umuhimu

wa elimu katika utetezi wa maadili katika jamii.

Ni muhimu hapa kusisitiza kuwa elimu ya kimaadili aipatayo mtu haina maana, kama hataitumia kuwanufaisha wengine. Ni wajibu wa mtetezi wa maadili kuchukua hatua ya kuwafunza wengine juu ya maadili. Hii ndiyo sababu Shaaban Robert anatumia kazi zake za kinathari kuwafunza maadili watu wa jamii yake. Hili ndilo lilokuwa lengo la kazi zake, na wala sio kujipatia fedha. Jambo hili linajitokeza vizuri zaidi katika tawasifu yake ya Maisha yangu na Baada ya Miaka Hamsini tunapoarifiwa namna alivyofaidika kidogo sana kifedha kutoka kwa kazi zake.

Nguli wa Kusadikika, Karama, anapoanzisha Uanasheria ni lazima yeye mwenyewe alikuwa amepata mafunzo ya Uanasheria. Haiwezekani kuwa angeweza kuanzisha taaluma asiyoielewa. Maarifa ya Karama katika Uanasheria yanadhihirika katika mzozo unaohusu tafsiri ya taaluma yenyewe. Tafsiri inayotolewa na mudir wa sheria haiwaridhishi watu. Hata mfalme mwenyewe anaonyesha kutoridhika. Kutoridhika kwa watu hawa kuhusu tafsiri ya mudir wa sheria ni ushahidi fika kuwa hakuwa ameyapata mafunzo ya uanasheria. Tafsiri ya Karama inawaridhisha watu wote; kumaanisha kuwa alikuwa mjuzi wa taaluma yenyewe.

Karama anapoanzisha taaluma yake ya Uanasheria, serikali inamwona kama alikuwa tone la mvua ambalo haliwezi kusababisha gharika. Lakini kwa kutumia maarifa, baadaye elimu yake inasambaa na kuwa tisho kwa serikali. Kuwa na wafuasi wengi ina maana kuwa watu walikuwa na imani kwa elimu ya Karama.

Pia usomi wa Karama unadhihirika kutokana namna anavyokinzana na dai potovu la waziri mkuu kuwa weusi wa nywele za Karama waonyesha ujinga wake. Kwa mujibu wa waziri mkuu, mtu mwenye mvi kichwani kama yeye, ndiye anayeweza kudai kuwa na hekima. Karama anasimama imara na kumfahamisha kuwa elimu ilipokuwa haijulikani duniani, mvi ziliheshabiwa kuwa alama ya hekima lakini wakati wake umepita na wala haziwi dalili ya chochote chenye maana. Kuna watu wengi wenye mvi ambao akilini mwao hamna ushauri uanaoweza kuokoa jamii.

Katika enzi hii tuliyo nayo, vijana walioelimika wanaweza kutoa mchango muhimu katika utetezi wa maadili. Mojawapo ya vitu vilivyofanya maadili kudidimia katika jamii, ni vijana kunyimwa nafasi kushiriki kikamilifu katika kushutumu maovu. Kutengwa huku kwa vijana kunawafanya kushiriki katika vitendo vinavyoudhi jamii.

Shaaban Robert anaashiria kuwa upotovu katika jamii hupata nafasi kwa mtu asiyeelimika. Mtu aliyeelimika daima hujaribu kukuza maadili. Katika kazi ya kinathari ya Adili na Nduguze. Adili sawa na Karama anaonekana mtu aliyeelimika. Wasifu wake waonyesha kuwa nafsi yake ilikuwa imehitimu katika mafunzo ya kimaadili. Baba yake alipofariki aliyaandaa mazishi yake na kutimiza mahitaji yote ya ada na desturi za kijamii.

Watu wote waliohudhuria mazishi hayo walitosheka na mipango mizuri aliyokuwa nayo. Hawakusita kumwona kama mtu aliyekamilika. Walipokuwa wakienda makwao, tunawaona wakisema kuwa, "Mwana wa Mhunzi asiposana huvukuta. Adili atakuwa mwema kama babake." (uk. 16). Adili anapopanga mazishi ya babake, ndugu zake hawapo karibu, na labda kifo cha baba yao hakikuwa na athari yoyote katika nafsi zao. Bila shaka

katika wakati huo walikuwa wakishiriki katika ulevi na anasa nyingine. Inaonkena kuwa tangu utoto wao hawakutenga wakati wa kujifunza mambo muhimu katika jamii yao.

Kwa kuonyesha umuhimu wa mtetezi wa maadili kuwafunza wengine, Shaaban Robert anatuonyesha namna, Karama baada ya kuelimika anajitwika mzigo wa kuwafunza Wasadiki wajibu wao wa kimaadili. Wao wanaonekana kuwa watu waliopotoka kiasi kuwa hawawezi kutambua kilicho adili na potofu. Wengi wao wanaposikia juu ya mashtaka ya Karama, wanaingiwa na wasiwasi na kumwona kama mtu mjinga aliyekosa mwelekeo. Wanashangaa ni kwa nini anataka kuhatarisha maisha yake. Lakini wale waliokuwa wameonja lengo na dhamira ya taaluma yake, wanamhesabu kuwa mtu bora asiyewahi kuonekana katika karne hiyo. Watu hao wanamtakia wokovu.

Pia katika kuonyesha umuhimu wa mafunzo, tunamwona Shaaban Robert akijitolea katika Adili na Nduguze kuwafunza watu wa jamii yake imani ya dini ya Kiislamu. Shaaban Robert akiwa mwislamu alikuwa akimwamini Mungu mmoja. Watu wengi wa jamii yake walikuwa wakiabudu mizimu. Jamii nyingi za Kiafrika, kabla hazikuwa zimeingiliana jamii za nje, na hata baada ya kuingiliana nazo; waliamini kuwa Mungu angeweza kufikiwa kupitia kwa mizimu. Wakati wa majanga kama vile njaa, mafuriko, mlipuko wa magonjwa na vita, jamii hizi za Kiafrika zingetoa dhabihu na maombi kwa Mungu kupitia kwa mizimu. Shaaban Robert anawaonya watu wa jamii yake kuwa kuabudu mizimu ni uasi unaomkasirisha Mwenyezi Mungu. Anawahimiza wamwabudu Mungu kupitia kwa mtume Mohammed.

Umuhimu wa mafunzo pia unadhihirishwa na Shaaban Robert kutokana na juhudi

anazofanya kuhakikisha kuwa Hasidi na Mwivu, ambao moyo na fahamu zao hazina maadili hata chembe wameelimika. Mafunzo kwao yanatolewa kwa ushirikiano wa Adili, Huria binti Kisasi (jini) na mfalme Rai. Shaaban Robert kupitia kwa Adili anatumia mbinu ya fasihi simulizi kwa kuwafanya Hasidi na Mwivu kusikiliza hadithi ya vitendo vyao viovu. Mbinu hii inaonekana kufaulu katika kupitisha mafunzo kwa walengwa, kwa sababu inapoendelea kutumika wanaaibikia matendo yao kwa kuziba nyuso zao.

Upotofu wa kina Hasidi ulikuwa umepita kiasi cha mipaka ya kibinadamu. Hata Huria binti kisasi hakufurahishwa nao. Anajitokeza kuwaelimu haja ya wao kuwa na utu:

> Kama mngalijua hatari ya kumtosa mtu, baharini, au mngalikuwa na fikira ya msiba, msingalijaribu kumtumbukiza ndugu yenu alipolala. Wauaji nyingi hamstahili kuishi (uk.50).

Ulimwengu wa majini waonekana kuwa makini kwa juhudi za mtu kutekeleza wajibu wa kimaadili. Mtu anayetenda mema anatuzwa, ilhali anayeasi anaadhibiwa. Mathalani juhudi za Adili za kuyaokoa maisha ya Huria alipoandamwa na nyoka, zinalipwa kwa maisha yake kuokolewa ndunguze wanapomtumbukiza majini. Zaidi ya hayo anapatiwa zawadi nyingine zenye thamani kubwa katika ulimwengu wa majini.

Kwa upande mwingine, adhabu wanayopewa kina Hasidi ni ya kucharazwa na kugeuza kuwa wanyama. Kuumbuliwa kuwa wanyama ni kutengwa na binadamu. Adhabu hii ina athari kubwa kisaikolojia. Katika kutengwa huku, mtu huwa amefarakana na jambo kubwa sana katika maisha ya binadamu - ushirikiano. Mtu ni kiumbe - jamii, na anapokuwa nje ya ukweli huo, hukaa katika hali ya upweke. Adhabu ya aina hivo igusayo

moyo wa mtu ni kali kuliko ile igusayo mwili tu.

Kama tulivyoona hapo nyuma, mfalme Rai anaelezwa kuwa mtu mwadilifu, anayependa kutoa mafunzo kwa kutumia mbinu ya utendaji. Yeye ni mmoja wa wanaonyesha jitihada za kuwafunza nduguze Adili maadili. Mfalme Rai anaonekana kupinga adhabu kama mbinu ya kufunzia na kutetea maadili. Anajitokeza kusisitiza kuwa badala ya adhabu kuongoa, inaumbua. Badala ya matumizi ya adhabu, anahimiza kuwa njia inayofaa ya kutoa mafunzo ya kimaadili ni ya kubadilishana mawazo au kushauriana. Haridhishwi na mbinu inayotumiwa na Huria, yenye lengo la kubadilisha uovu wa Hasidi na Mwivu. Kile mbinu hiyo inachokifanya ni kukuza mateso.

Katika kazi zake za kinathari, Shaaban Robert anahimiza kuwa njia bora ya kuleta mabadiliko ni kupitia kwa mashauriano. Sababu hii ndiyo inayomfanya kupitia kwa mfalme Rai kuanzisha juhudi za mapatano kati ya ulimwengu wa majini, wanyama na binadamu. Jitihada hizi zinakusudiwa kuwafanya Hasidi na Mwivu binadamu tena, ndipo atumie mbinu yake ya mashauriano kuwaonya dhidi ya uovu. Rai anaandika barua kwenda ulimwengu wa majini na kusihi kuwa nduguze Adili warudishiwe utu. Juhudi zake zinafanikiwa.

Wanaporudishiwa utu, Rai anaanzisha mafunzo ya kimaadili kwa Hasidi na Mwivu. Anawaonya: Kama wavivu, walijitahidi kuwa hodari, ilikuwa kinyume hodari kuwa wavivu; kama waovu walitaka kuwa wema, ilichukiza wema kuwa waovu; kama maskini walitafuta utajiri, ilikuwa ujinga matajiri kufuja walichokuwa nacho; kama mbegu kidogo iliongezwa mchanga, ilikuwa uharabu mtu kuua ndugu yake (uk. 62).

Mbinu hii ya mfalme Rai inafaulu kugeuza upotofu wa kina Hasidi na tangu wakati huo wanabakia kuwa waadilifu katika maisha yao yote.

Utoaji wa mafunzo kwa wapofu ni hatua muhimu katika kufufua maadili. Watetezi wa maadili inafaa waunganishe jitihada na maarifa yao iwapo wanataka kuumba jamii mpya. Kama sio jitihada za Adili, Rai na Huria, labda Hasidi na Mwivu wangezidi kuzama katika maovu.

Nguvu za elimu katika kufufua maadili, pia zadhihirika katika kazi ya kinathari ya Kusadikika. Jitihada za Karama na zile za wajumbe zinahimiza nchi ya Kusadikika kubadilisha mienendo miovu. Nchi iliyokuwa imechanganyikiwa kimaadili, inapokubali mabadiliko ya kina Karama inachukua sura mpya. Zamani ilikuwa imeoza na kuozeana. Kwa mfano, mwanamke mmoja angeweza kuolewa na wanaume wengi. Pia raia walikuwa wakishiriki katika maovu mengine. Wajumbe wote wanashiriki katika kuwafunza raia umuhimu wa yale waliyojifunza katika maeneo waliyoyatembelea. Mjumbe wa mbinguni, Ridhaa, kwa mfano, anawalaumu Wasadi kwa desturi yao mbaya ya kutafuta fimbo baada na wala sio kabla ya kuumwa na nyoka.

Kile Ridhaa anachomaanisha na kuumwa na nyoka ni kushiriki katika maovu. Ridhaa anawafahamisha kuwa wamekuwa wakishiriki katika maovu kwa muda mrefu na hakuna faida wayoipata ila hasara, huzuni na kilio siku zote. Ridhaa anawahimiza kuwa ni lazima sasa maovu yabadilishwe kwa mema. Ushawishi huu na ule wa wajumbe wengine baadaye unaitikiwa na nchi, na kuipatia ufanisi mkubwa.

Karama pamoja wale wajumbe sita wanatoa uchochezi kwa watetezi wa maadili. Ingawa mafunzo yao awali yalipingwa na nchi ya Kusadikika baadaye yanakubaliwa. Hali hii inawafahamisha watetezi kuwa subira ni kitu cha lazima katika mafunzo yao ya kimaadili.

## 4.2.0. USHUJAA

Kazi za kinathari za Shaaban Robert pia zinaonyesha kuwa ushujaa in nguzo muhimu katika utetezi wa maadili. Kwa kutumia jicho la akilini, utetezi wa maadili unaweza kuangaliwa kama aina fulani ya vita au safari inayohitaji maandalizi mwafaka. Hatari zilizomo katika utetezi wa maadili zinaelezekea vizuri katika shairi la A. Abdalla liitwalo Wasafiri Tuamkeni [2]

Abdalla anawakumbusha watetezi wa maadili kuwa, utetezi wa maadili ni aina ya safari yenye miiba ya sumu njiani. Zaidi ya miiba, safari hiyo imejaa wanyama wa mwito wakali, walio tayari kukinasa kitu chochote wakionacho. Aidha anasisitiza kuwa njiani mtu anakumbana na bahari pana yenye kina kirefu, iliyojaa mawimbi yenye nguvu. Abdalla anawapa moyo watetezi kuwa ingawa watakumbwa na matatizo hayo yote mwishowe kuna faraja.

Vita vyovyote vinahitaji ujasiri. Ujasiri unakuwa kama ngao. Katika hali ya maisha kuna aina mbili za ushujaa: wa nguvu na silaha; na wa nafsi. Kwa ushujaa wa kwanza, mtu hutegemea silaha, silaha hizo zikipotea mtu hawezi kuendelea mbele. Lakini katika ushujaa wa pili, mtu anajiamini mwenyewe na kwa vyovyote vile atazidi kwenda mbele. Katika utetezi wa maadili, ushujaa wa aina ya pili ndio muhimu. Umuhimu wake unatokana na

ukweli kuwa hakuna kikwazo chochote kinachoweza kuwa pingamizi kwa mtetezi wa maadili

Kazi za kinathari za Shaaban Robert ni kwasi katika kutuhimiza na kutuchorea mazingira ambapo ushujaa umefaulu katika kubadilisha hali zilizokuwa zimeoza kimaadili. Shaaban Robert anawahimiza umma kujitolea muhanga namna alivyofanya ili kuleta mabadiliko yanayofaa katika jamii. Nguli katika kazi zake za kinathari wamechorwa kuwa mashujaa, na ushujaa huo umewawezesha kufufua maadili katika jamii husika. Katika Kusadikika, kwa mfano, Karama anatumia moyo wa kishujaa kama silaha ya kupinga maongozi ya kiimla katika nchi yake. Baadhi ya wasiri wake hata hawakuwa wanajua kuwa alikuwa na silaha hiyo mpaka walipomwona akiitumia katika utetezi wake.

Kwa hakika, Karama anajitokeza kuwa shujaa kwa vile katika nchi yake kulikuwa na sheria iliyopinga vikali nia ya mtu kuwa na ndoto ya kuanzisha taaluma yoyote bila ya kibali cha serikali. Alikuwa ana uhakika kuwa hata kama angeulizia ruhusa hangeweza kusikizwa. Kutokana na wasifu tuliopewa wa Karama, yeye alikuwa mmoja wa watu waliokandamizwa, na hivyo basi haingeweza kuwa rahisi kusikizwa na viongozi katili. Hii ndiyo sababu, bila kujali sheria dhalimu, anapiga hatua ya kuanzisha uanasheria bila kushauriana na serikali.

Kitendo cha Karama kuanzisha Uanasheria kilionekana kuwa, haramu kwa mujibu wa serikali, kwa sababu taaluma kama hii ilikusudiwa kuanziashwa na watu wenye nasaba bora kama vile wafalme, madiwani na viongozi wengine na wala sio watu duni kama Karama.

Serikali inashikilia kuwa mambo makubwa yaidhinishwe na viongozi kama njia ya kuzima upinzani kutoka kwa wadhulumiwa. Serikali ni lazima ilikuwa inayafahamu mashaka yanayompata mtu mwerevu wakati aliye mjinga anapoerevuka. Inaonekana kupinga jitihada zozote za kuleta mabadiliko. Kwa mfano, Majivuno anasisitiza kuwa haidhaniwi kuwa ruhusa ingetolewa ya utaalamu mwingine zaidi ya kusadiki kwa vijana wa nchi hiyo ungeleta faida yoyote kwao.

Majivuno anashangazwa na ujasiri alio nao Karama katika harakati za kuleta mabadiliko. Analalamika kuwa karama alipoulizwa kama alikuwa mwalimu wa uanasheria alikubali upesi kama alitunukiwa hadhi kubwa. Hofu hii ndiyo inayomfanya atake kumwangamiza kwa sababu anabashiri kuwa akiachwa kwendeleza taaluma yake, kisha angeendelea kudai haki zake hadi afikie kupigania ufalme.

Hatua ya Karama kushua uanasheria katika mazingira yenye uhasama, ni jambo linalohitaji kujitolea nafsi. Karama hawi kama binadamu wengi wenye tabia ya kujikalia na kuwangojea wengine kuanzisha mambo. Wanapoona mambo hayo yameanza kuonyesha ufanisi, ndipo wanajitokeza na najisi zao za mashambulizi. Ujasiri huu wa Karama kuanzisha juhudi za kuikomboa jamii iliyopotoka ni changamoto muhimu kwa watu wa jamii zetu, kuwa wasiwe watazamaji wa maovu yanayolemeza jamii, bali wawe watendaji. Bila kuwa watendaji, hakuna wokovu wa kupoza jamii yetu.

Aidha kigezo cha ushujaa ndicho kinachofanikisha safari za wajumbe wa Kusadikika. Safari zao zilikuwa zenye majaribu magumu. Mtu alikuwa anatoka katika nchi anayoijua na kuelekea kwa nyingine asiyoijua kabisa. Msafiri hakuwa anajua kama

mbeleni alikuwa akingojewa na msaada au maangamizo. Fauka ya hayo, safari hizi zilikuwa ndefu ajabu zilizopitia misituni, nyikani kwenye ukiwa na jangwani kwenye kiu.

Sio mtu wa kawaida anayeweza kuwa na ari ya kufanya safari za aina hii. Ni lazima mtu huyo awe shujaa. Wajumbe wengine waliondoka katika nchi yao wakiwa vijana na waliporudi walikuwa wazee. Wakiwa safarini, walijaribiwa kwa kila taabu, mathalani njaa, kiu, ukiwa na ukatili. Hawakusita kwenda mbele kwa uchungu wa shida wala hawakughairi kurudi kwao kwa tamu na anasa. Kwa kujitolea dhabihu, walikuwa wameyaweka maslahi ya jamii yao mbele ya kusahau maslahi yao ya kibinafsi.

Wengi wa wajumbe hawa wanakutana na kifo kikiwa kimewakodolea macho, lakini wanapiga moyo konde. Kwa mfano, Kabuli, mjumbe wa Kusini ananusurika kifo mara mbili: mara ya kwanza ananusurika kuliwa na mfalme Jeta wa nchi ya Juju, na mara ya pili alipofika katika nchi ya Hasira. Katika nchi ya Hasira anashtakiwa kwa ujasusi na kuhukumiwa kulichimba kaburi lake mwenyewe, na likisha kuwa tayari ajilaze juu ya ukingo wake ili shingo lake likerezwe kwa msumeno. Kwa kimwujiza, johari analolipata akiwa analichimba kaburi linamwokoa. Askari waliomlinda wanaanza kuling'ang'nia johari na kujiingiza kaburini. Kabuli anatumia nafasi hiyo kutoroka.

Katika riwaya ya Utubora Mkulima, Utubora ni jasiri kwa kutetea kile Shaaban Robert anachokiamini kuwa adili. Hatua ya Utubora kufikia uamuzi wa kuacha kazi yake ya ukarani na kuingilia nyingine asiyokuwa na ujuzi nayo inahitaji ujasiri. Ushupavu mwingine wa Utubora katika utetezi wa maadili, unajitokeza pale yeye na Radhia wanapinga tabia ya kuhusisha ndoa na mali. Sheha, na wazazi wake Radhia wanathamini

mali katika ndoa. Hii ndiyo sababu Sheha anamwacha Utubora na kuolewa na tajiri. Nao wazazi wake Radhia wanatarajia binti yao kuolewa na mtu mwenye mali. Maadam Makuu ana mali, wanakubali posa lake.

Radhia anajasiri kuuvunja uchumba na Makuu na kukubali kuolewa na Utubora aliye kijana maskini. Vijana hawa wawili wanaridhiana kuwa kufu wa kuoana licha ya tofauti ya mali baina yao. Uamuzi wa Radhia kuolewa na utubora unakuwa pigo kubwa kwa wazazi wake. Wazazi wake Radhia wanaonekana kuwa sampuli ya watu wanaowachukulia mabinti wao kama vitega uchumi. Inapofikia wakati mabinti hawa wanataka kuolewa, wazazi hao wanadai mahari ya kiwango cha juu kana kuwa wanawauza. Vijana hawa wawili wanapinga na kutoa funzo kwa wazazi wenye tabia hiyo mbovu.

Katika kazi ya kinathari ya Kufikirika, Utubusara anajitokeza kuwa shujaa kwa kuingiza mambo mapya katika mfumo wa kijamii uliopinga mabadiliko. Utubusara anajasiri kuhimiza kuwa mabadiliko katika jamii ni jambo la lazima. Anaonekana kupinga mila na desturi zilizopitwa na wakati kama vile kafara ya binadamu. Ufanisi wa mambo ya kigeni unaonyeshwa na Utubusara wakati mapendekezo yake kuwa mtoto angepelekwa hospitalini angepona. Hali kadhalika, ujasiri wa Utubusara unaonekana pale anapopinga kigezo kilichotumiwa kumchagua kama mtu mjinga na mfanya biashara kama mtu mwerevu. Ni kutokana na ujasiri, tunamwona akijitetea mpaka mwishowe anajinusuru na kumnusuru mwenzake.

Na katika riwaya ya Siku ya Watenzi Wote, Shaaban Robert anapendekeza kuwa

matatizo yanayoikumba jamii yangetatuliwa iwapo dini zingejasiri kuungana. Utengano wa dini unaonekana kuwa aina ya upotovu kwa sababu sheria ya Mungu ni moja na hivyo basi binadamu hawana budi kumwendea wakiwa katika fungu moja.

Katika riwaya hii pia, Shaaban Robert anajutia hali ya wanawake. Wanawake katika jamii yake wanakandamizwa. Anawashauri wanawake hao kuwa hali yao ingebadilika kama wangetupilia mbali woga wa zamani kuwa wajibu wao ni kuwa watiifu kwa jamii. Anawahimiza wawe jasiri kwa kuasi vitendo viovu wanavyofanyiwa na mifumo katili ya kijamii inayowapa wanaume nguvu za kuwanyanyasa. Anaonyesha kuwa wanatakiwa kuwa na ujasiri kama ule unaonyeshwa na wasichana, Zena na Sarah wanapomkabili mla riba kukomboa sufuria za kimbaumbau. Wanawake pia wanashauriwa kujasiri kwa kujiangua kutoka mabuibui zao na kuanza kutafuta fursa ya uchaguzi katika serikali. Wakishika madaraka, wao wenyewe wangekuwa katika hali nzuri kujitetea kuliko kuwategemea wanaume.

## 4.3.0. MOYO MWEMA

Kazi za kinathari za Shaaban Robert zinaonyesha pia kuwa utetezi wa kimaadili unahitaji moyo mwema uliotayari kupokea mambo kwa subira. Shaaban Robert anaonyesha kuwa hii ni nguzo muhimu kupitia wahusika kama Adili. Adili anajitokeza kuwa na moyo mwema. Wakati ndungu zake wanamjia wakiwa hoi, moyo wake unawaka moto kwa huzuni. Unasikitikia hali yao na unamfanya Adili kuwakimu mahitaji yao ya kimwili na kiroho. Anawalisha, kuwavalisha na kuomba dua kuwa yeye na ndugu zake wabarikiwe. Licha ya hayo, moyo wake unamwongoza kuwaonya juu ya hatari za ulevi na uvivu. Tunaweza kusema kuwa Adili anayafanya haya yote kwa sababu moyo wake

ulikuwa na mapenzi makubwa juu ya ndugu zake. aliwapenda kama pumzi ya maisha yake mwenyewe.

Adili na nduguze wanapofanya safari ya kibiashara, jahazi lao linatia nanga ili mabaharia wapate kutafuta vyakula na maji. Adili anapotoka nje anamwona tandu akifukuzwa na nyoka. Tandu anapotoa mlio wa kusikitisha, moyo wake unaingiwa na huruma. Moyo wake unashindwa kuvumilia na ndipo anaokota jiwe na kumponda nyoka kichwani.

Moyo wake Adili ni imara katika kuonyesha mapenzi na huruma kwa ndugu zake hata wakati ukatili wao umefikia kileleni. Anapojaliwa mali katika Mji wa Mawe ni nia yake kugawana na nduguze. Aidha, anapookolewa na Huria kutoka majini; na Huria anapendekeza adhabu ya kifo dhidi ya nduguze, moyo wake unaingiwa na huruma na kusihi kuwa wasamehewe. Moyo huu wa Adili unathibitisha ukweli wa msemo kuwa, damu ni nzito kuliko maji. Binadamu wa moyo wa kawaida angetumia nafasi hiyo kulipiza kisasi. Moyo unaonyeshwa na Adili hauko mbali na ule ulioonyeshwa na Bwana Yesu alipokuwa msalabani. Alizidi kuwaombea maadui zake msamaha.

Moyo wake Adili sio tu kiti cha upendo na huruma, bali pia chanzo cha ustahamilivu na ushupavu ambavyo ni elementi muhimu katika utetezi wa maadili. Ni kutokana na moyo wa ushupavu, Adili anapata nyota ya jaha katika Mji wa Mawe. Ndungu zake wanapoogopa, uimara wa moyo wake unamfanya ajaribu kujiokoa kabla ya kupoteza matumaini.

Hali kadhalika, ndugu zake wanapomtumbukiza majini, ushupavu wa moyo ndio unaomwokoa. Anajidhihirika kutokuwa mtu wa kukata tamaa, alipokuwa majini na kabla pumzi yake haijakwisha, anakusudia kuepuka. Jaribu lake linakutana na fanaka maana kabla moyo wake haujakoma, anajiona akielea juu ya bahari.

Hali kadhalika, ni moyo wenye subira unaomzuia Adili kukata tamaa juu ya maovu ya ndugu zake. Ingawa ndugu zake wanazidi kuzama katika vitendo vipotovu, moyo wake bado una matumaini:

> Alikaribia kukata tamaa, lakini alitahayari mwenyewe alipojiona kwamba alikuwa maskini wa Subira... Alitingisha kichwa chake kama aliyekuwa akikataa wazo la kukata tamaa (uk. 58).

Inavyoonekana ni kuwa, moyo wa Adili ndio steringi ya utetezi wake wa kimaadili. Moyo wake unahitilafiana sana na mioyo ya watu wengine. Kigezo hiki cha moyo shupavu ndicho kinachomfanya kuwa mshindi katika vita vyake dhidi ya maovu.

Kigezo hiki cha moyo pia ni muhimu katika kuelewa ushupavu wa Karama katika <u>Kusadikika</u>. Moyo wake ndio asili na chemchemi ya ushujaa na sifa nyinginezo za kimaadili. Ingawa ameshtakiwa na kuingizwa gerezani bado moyo wake una tumaini kuwa angeokoka. Moyo wake Karama hauko mbali na ile ya wajumbe sita wa Kusadikika. Wao pia walikuwa na mioyo ya kustahimili. Tumeona namna walivyokumbwa na dhiki ya kila namna lakini mioyo yao haikulegea. Walikazana kwenda mbele mpaka walipofikia malengo ya safari zao.

Katika sura hii tumeyadili mambo matatu ambayo tunayaona kama nguzo muhimu

zinazomchochea Shaaban Robert kuendeleza vita, vyake dhidi ya maovu katika jamii. Bila ya elimu, ushujaa na moyo shupavu, vita vya shaaban Robert havingefikia popote kwa sababu anaendesha utetezi wake katika mazingira yenye uhasama. Mambo haya yanabakia kama mwongozo kwa watetezi wa maadili wa wakati wote .

**TANBIHI**

1. Matteru, M. L. (1975) MULIKA uk. 30

2. Abdalla, A. (1973) Sauti ya Dhiki uk. 67

## SURA YA TANO

### 5.0.0. HITIMISHO

Katika sura hii tumetoa hitimisho ya utafiti wetu. Sura yenyewe ina sehemu tatu muhimu. Sehemu ya kwanza inabeba muhtasari wa utafiti, ya pili, inazungumzia utoshelevu wa nadharia tulivyoitumia na ya tatu ni ya mapendekezo.

### 5.1.0. MUHTASARI WA MATOKEO

Utafiti wetu ulikuwa na Shabaha tatu. Shabaha ya kwanza ilihusu kutambua aina za maadili yanayoshughulikiwa na Shaaban Robert katika kazi zake za kinathari. Katika utafiti wetu tumegundua kuwa Shaaban Robert ameshughulikia aina tatu muhimu za maadili katika kazi zake za kinathari. Aina ya kwanza anayoshughulikia ni ya kisiasa. Anajitokeza kuhimiza usawa wa kisiasa, na kupinga mfumo wa kisiasa unaowakandamiza wanyonge. Shaaban Robert anashutumu siasa za dhuluma kutokana na tajriba aliyokuwa nayo, nchi yake ya Tanzania ilipotawaliwa an Wajerumani na baadaye Waingereza.

Serikali za kikoloni zilijulikana kuwa na tabia ya kuwanyima Waafrika haki zao za kisiasa, kama vile utoaji wa maamuzi ya sera zilizogusia maisha ya kila siku ya raia. Hali hiyo iliwakera wananchi wa Tanzania na wakaanza kujiunga katika makundi ya kisiasa kama vile Tanganyika Africa Association (KAA) na Tanganyika Africa National Union (TANU) wakiwa na lengo la kujinyakulia uhuru. Baadaye shinikizo kutoka kwa makundi hayo ya kisiasa zililazimisha serikali za kikoloni kutoa uhuru kwa wananchi wa Tanzania.

Aina ya pili ya maadali yanayoshughulikiwa na Shaaban Robert katika kazi zake za kinathari ni ya kiuchumi. Mwandishi huyu alisikitikia hali ya kiuchumi aliyoshuhudia nchini mwake. Nyenzo za kuzalisha mali zilikuwa mikononi mwa watu wachache, hasa wakoloni. Waafrika waliokuwa wengi walizidi kuangamia katika umaskini, njaa na magonjwa. Serikali ya kikoloni ilikuwa inaipora nchi ya Tanzania malighafi yake na kuitumia kuendeleza nchi zao za Kimagharibi. Kwa mfano, katika Kusadikika tunaarifiwa na mjumbe wa Magharibi, Buruhani juu ya maendeleo aliyoyaona kule: Miji mikubwa na majengo ya aushi; mabarabara yaliyosakifiwa na madaraja ya ajabu; utabibu wa watu na wanyama...

Kwa upande mwingine, uwekevu wa nchi ya Tanzania ulikuwa na walakini. Katika kusawazisha hali, Shaaban Robert anazihimiza nchi na watu matajiri kuwa na ukarimu kwa watu na nchi ya Tanzania. Anashauri kuwa michango yao ingeweza kupitia kwa mashirika kama lile la 'Jumuia ya Adili' linalopendekezwa katika riwaya ya Siku ya Watenzi Wote. Hofu yake ni kuwa misaada hiyo ikitolewa kwa watu binafsi, huenda ikakosa kuwafikia watu waliokusudiwa.

Maskini nao wanahimizwa kutia bidii katika miradi yao yenye lengo la kuinua hali yao ya kiuchumi. Anawahimiza kupitia kwa bidii zinazoonyeshwa na mfalme Rai pamoja na wajumbe wa Kusadikika ambao, juhudi zao zilichangia maendeleo ya nchi zao.

Shaaban Robert pia anashughulikia maadili ya kijamii, katika kazi zake za kinathari. Jamii ya Shaaban Robert ilikuwa imejengeka katika misingi ya kitabaka. Anatoa wito kwa watu wa jamii yake, na jamii ya Kiafrika kwa jumla kuungana. Wito huu wa muungano unadhihirika katika kazi yake ya kinathari ya Siku ya Watenzi Wote ambapo anayahimiza

makundi ya kidini kuungana. Kwa maono yake jamii ilivyotengana huyapatia maovu nafasi ya kusambaa na kuozesha jamii.

Hali kadhalika, Shaaban Robert anajitokeza kupinga ada na mila zinazosambaratisha jamii katika misingi ya kijinsia. Wanawake na wanaume wanapaswa kupewa nafasi sawa na jamii ndiposa washiriki kikamilifu katika utetezi wa maadili. Pia anahimiza kuwa na sheria zisizowabagua watu kwa misingi ya kijinsia au kihadhi bali zinazowaangalia kwa jicho lisilopendelea.

Shabaha yetu ya pili katika utafiti huu, ilikuwa kueleza jinsi Shaaban Robert alivyotumia uhusika kuwasilishia utetezi wake wa kimaadili katika kazi zake za kinathari. Tumegundua kuwa kwa kiasi kikubwa, Shaaban Robert ametumia uhusika wa kiistiara. Kuna wahusika waadilifu na waovu. Sifa za kimaadili au za uovu zimeashiriwa katika majina walivyopewa. Kwa mfano, kuna wahusika kama vile Adili, Utubora na Utubusara ambao tabia na matendo yao yanaonyesha uadilifu, ilhali kuna wengine kama vile Hasidi na Mwivu wanaonyesha uovu na upotofu katika tabia na matendo yao.

Katika matumizi ya wahusika wa kitaashira, Shaaban Robert anataka kuonyesha vita vilivyoko kati ya maadili na maovu. Katika mgogoro huo, inadhihirika kuwa maadili yana nguvu nyingi dhidi ya maovu. Hii inatokana na uwezo wa matendo mema kuyashinda yale yaliyo maovu.

Shabaha yetu ya tatu ilikuwa kufafanua nguzo muhimu zinazoongoza utetezi wa

maadili katika kazi za kinathari za Shaaban Robert. Tumegundua kuwa utetezi wa maadili wa mwandishi huyo umejengeka katika nguzo tatu. Nguzo ya kwanza ni ya mafunzo. Mwandishi huyu amedhihirisha kuwa vita dhidi ya maovu haviwezi kufua dafu iwapo mtetezi hajapata elimu ya kimaadili, na apiga hatua ya kuwafunza watu waliopotoka, haja ya kubadilisha matendo yao. Nguzo ya pili ni ya ujasiri. Tumegundua kuwa utetezi wa maadili ni aina ya vita vinavyohitaji ujasiri. Ujasiri unaohitajika sio wa nguvu za kimwili na silaha za kivita, bali wa nafsi. Nguzo ya mwisho na inayohusiana na ya pili ni ya moyo shupavu wenye subira na uvumilivu. Subira na uvumilivu vikikosa, mtetezi hutetereka njiani.

## 5.2.0. UTOSHELEVU WA NADHARIA

Nadharia tuliyotumia ya kisosholojia inafaa katika kazi za kinathari za Shaaban Robert. Shaaban Robert anajitokeza kuwa mwandishi aliyejitokeza kuhudumia jamii. Kwa mfano, katika riwaya ya <u>Siku ya Watenzi Wote</u>, ambayo tunaweza kuiona kama kilele cha kazi zake za kinathari , mwandishi huyu anayamulikia matatizo yaliyokuwemo katika jamii yake. Matatizo makubwa yanayojitokeza ni jamii yenye matabaka, umaskini na ukandamizaji wa wanawake.

Shaaban Robert anashiriki katika utatuzi wa matatizo haya kupitia kwa pendekezo lake la muungano wa kidini: Uislamu na Ukristo. Anaonekana kuamini kuwa muungano huu wa kidini ungekuwa jukwaa la kuondoa na pia kuunganisha ulimwengu mzima. Muungano huo ungekuwa na nguvu za kutawala tofauti za kisiasa, kiuchumi na kikabila. Halafu watu wangeishi katika upendo, amani na furaha.[1]

Kasoro tunayoiona katika mapendekezo yanayotolewa na Shaaban Robert kwa matatizo yanayoikumba jamii yake ni kuwa, hafafanui namna mapendekezo hayo yangeweza kutekelezwa. Kwa mfano, 'Jumuia ya Adili' tunayoiona ikiongozwa na kijana Ayubu imebana shughuli zake jijini; na hatuonyeshwi namna ingesambaa mashambani. Aidha hatuonyeshwi mkakati ambao Jumuia ya Adili ingetumia kuondoa umaskini, matabaka na ukandamizaji wa wanawake. Ingawa tunaona Jumuia ya Adili ikifanya juhudi za kuwasaidia maskini kwa hali na mali, lakini tunawaona maskini wakibakia kuwa maskini na matajiri wakiendelea kuwa matajiri.

UNIVERSITY OF NAIROBI
EAST AFRICANA COLLECTION

Suluhisho la kiutendaji ambalo tungetarajia Shaaban Robert kulitoa katika utatuzi wa shida katika nchi yake ya Tanzania na nchi nyingine changa ni utawala mwema, upanuzi wa kiuchumi na ugawaji wa rasilimali kwa njia ya haki. Lakini hata hivyo jitihada za Shaaban Robert kuhudumia jamii yake zinastahili kupongezwa.

## 5.3.0. MAPENDEKEZO

Katika utafiti huu tumelishughulikia swala la utetezi wa maadili katika fasihi nathari ya Shaaban Robert, na upeo wetu ulijikita katika kazi za kinathari tano tu. Kuna haja ya utafiti zaidi kufanyiwa utetezi wa kimaadili katika kazi nyingine za mwandhishi huyu ambazo hatukuweza kuzishughulikia; na pia utafiti zaidi wahitajika juu ya namna Shaaban Robert anavyotetea maadili katika tanzu nyingine kama vile ushairi.

Isitoshe, kama haja ya utafiti kufanyiwa fani katika kazi za kinathari za Shaaban Robert.

**TANBIHI**

1. Mulokozi M. M. (1980) Viewpoints: Essays on Literature and Drama uk. 30

## MAREJELEO


Abdalla. A. (1973) Sauti ya Dhiki (Oxford University Press: Nariobi)

Bertoncini. E. Z., (1989) OUTLINE OF SWAHILI: Prose Fiction and Drama (E. J. Brill: Leiden)

Biblia Takatifu pamoja na Koran

Brenn. E. W. (1973) Mazungumzo ya Alfa Lela Ulela (Longman: Nairobi)

Carrol. D. (1980) Chinua Achebe (The Macmillan Press Limited: London)

Escarpit. R. (1971) Sociology of Literature (Frank and Cass: London)

Ferm. V. (1957) Encyclopeadia of Morals (Peter Owen Limited: London)

Gachukia. E (1980) The Cultural Conflicts In the EAst AFrican Literature (Unpublished. Phd Thesis. Unversity of Nairobi)

Gibbe. G. A. (1980) Shaaban Robert: Mshairi (Tanzania publishing House: Dar es Salaam)

Masoko. D na Mdee. J. (1984) MULIKA (Taasis ya Uchunguzi wa Kiswahili: Dar es Salaam)

Matteru. M. L. (1975) MULIKA (Taasis ya Uchunguzi wa Kiswahili: Dar es Salaam)

Mbatiah. A. M. (1999) The Origin and Development of the Swahili Thesis Novel in Tanzania (Unpublished. PhD thesis. university of Nairobi)

Mbughuni. P. (1978) From Oral to Written: The Politicization of Kiswahili Literature in Tanzania (Unpublished PhD thesis. Indiana University)

Mulokozi. M. M. (1980) "Two Utopia: A comparative Examinmation of William Morris. " In viewpoints: Essays on Literature and Drama (Kenya Literature Bureau: Nariobi)

Njogu. K. W. (1986) "Falsafa ya Shaaban Robert katika Riwaya Zake". MWAMKO (Chuo Kikuu cha Nairobi: Nairobi)

Robert. S. (1966) Kusadikika (Thomas Nelson and Sons Limited: London)

_________ (1966) Kufikirika (Thomas Nelson and Sons Limited: London)

_________ (1966) Ashiki Kitabu Hiki (Thomas Nelson and Sons Limited :London)

_________ (1968) Adili va Nduguze (Thomas and Nelson and Sons Limited: London

_________ (1968) Utubora Mkulima (Thomas Nelson and Sons Limited: London)

__________ (1968) Siku ya Watenzi Wote (Thomas Nelson and Sons Limited: London)

__________ (1968) Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini (Thomas Nelson and Sons Limited: London)

Sengo, T.S.Y. (1973) Katika Temu C. W. na Kiango S. D. (Wahariri) KISWAHILI (Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili: Dar es Salaam)

Shifa, A. N. (1971) In Topan F. M. (Mhariri) Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili (Oxford University Press: Dar es Salaam)

Taasis ya Uchunguzi wa Kiswahili (1981) Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Oxford University Press: Dar es Salaam)

Taiwo, O. (1986) Social Experiences In African Literature (Forth Dimension Publishers: Enugu)

Thiong'o, N. W. (1978) "Literature in Society" In Gachukia E and Akivaga E. (Wahariri) Teaching of AFrican Literature in Schools (Kenya Literature: Bureau Nairobi)

Wafula, R M. (1989) The Use of Allegory In Shaaban Roberts Prose works (Unpublished. M. A. Thesis, Unviersity of Nairobi)